SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



## Madhila ya mtoto anayebakwa na 'sauti' ya baba

UKURASA 18




## LWANDAMINA KUAMUA HATIMA YA DUBE

UKURASA 23

Nipashe Jumapili
MWANGA WA JAMII
Jumapili Desemba 5, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0580785
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Samia: Kuna kundi linaichafua serikali

UKURASA 2




## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### BASI LILIVYOTEKETEA, KUUA, KUJERUHI 19

MTU mmoja ambaye jina lake halijafamika raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), amefariki dunia na wengine...

## Wataalamu waonya kuhusu upotoshaji wa chanjo ya corona

UKURASA 2



### UAMUZI MGUMU WA UMMY

## Mbinu tisa za shule binafsi kushikilia watoto saa nyingi

UKURASA 4

MICHEZO SIMBA KUMALIZA KAZI ZAMBIA LEO UK.24
MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA



Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu Ardhi (ARU), Balozi Salome Sijaona (wa pili kulia), akimvisha kofia Jaji Mkuu mstaafu Mohamed Chande Othman kama ishara ya kumsimika rasmi kuwa Mkuu wa Chuo Kikuu hicho, wakati wa mahafali ya 15 ya chuo hicho, mkoani Dar es Salaam jana. Kulia ni Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Evaristo Liwa na (kushoto) ni Naibu Makamu Mkuu wa chuo (Taaluma), Prof. Grabriel Kassaga. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wataalamu watoa angalizo upotoshaji chanjo ya corona

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WATAALAMU wa afya wametoa angalizo kwa wananchi dhidi ya upotoshaji unaofanywa na baadhi ya watu kuhusu usalama wa chanjo za ugonjwa wa UVIKO-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Wamesema kuna haja wananchi kujitokeza kwa wingi kupata chanjo ya UVIKO-19 kwa kuwa imeidhinishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba nchini (TMDA) kuwa ni salama kwa watu wote, wakiwamo wenye magonjwa ya muda mrefu.

Angalizo hilo lilitolewa jana wakati wa semina kwa wanahabari na watu mashuhuri kuhusu afua za kinga dhidi ya tishio la wimbi la nne la UVIKO-19 na uhamasishaji wa chanjo hiyo iliyofanyika kwa njia ya mtandao.

Profesa wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Deodatus Kakoko, alisema kuwa wajawazito hawakushirikishwa kwenye majaribio ya dawa, taarifa za usalama wao bado zinafanyiwa utafiti ingawa wajawazito wameonekana kuwa katika hatari kubwa ya kupata ugonjwa huo, hivyo waendelee kuchukua tahadhari kwa kuepuka mikusanyiko isiyokuwa na maana.

Prof. Kakoko alisema hakuna tatizo kwa kinamama wanaonyonyesha kupata chanjo ya UVIKO-19 na anashauriwa kuendelea kunyonyesha vyema hata kama amepata chanjo hiyo.

Mtaalamu huyo wa afya pia alisema mgonjwa mwenye kisukari na mwenye Virusi vya Ukimwi (VVU) anaweza kupata chanjo hiyo kwa sababu inaongeza kinga mwilini na inaweza kumsaidia kuongeza kinga na kupunguza kabisa maambukizi hayo. Prof. Kakoko aliwataka vijana wanaosambaza taarifa za upotoshaji kwenye mitandao ya kijamii juu ya chanjo hiyo, waache mara moja kwa kuwa kwa sasa serikali inaendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali na itakapomaliza ilhali uvumi ukiendelea, wataanza kuchukuliwa hatua za kisheria.

"Mwanzo wizara ilitaka kuanza kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanavumisha taarifa za chanjo, tukashauri tuendelee kutoa elimu kabla ya kuanza kuwachukulia hatua, hivyo ninawataka vijana waache na wajitokeze kupata chanjo hii kwa sababu wao ndio taifa la kesho," alisema Prof. Kakoko.

Katika mkutano huo wa mtandaoni, Mchungaji Daniel Mgogo, aliwataka viongozi wenzake wa kiroho kuepuka mahubiri yenye lengo la kupotosha kuhusu chanjo ya corona badala yake wajikite kwenye taarifa sahihi zinazotoka kwa wataalamu wa afya. Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, aliwataka waandishi wa habari kutumia vyema kalamu zao kufikisha elimu ya umuhimu wa chanjo ya corona kwa wananchi ili kupunguza maambukizi ya ugonjwa wa UVIKO-19 nchini.

Msigwa alisema msimamo wa sasa wa serikali dhidi ya COVID-19 ni kujikita kwa maelekezo ya wataalamu wa afya na si vinginevyo.

# Samia: Kuna kundi linaichafua serikali

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema kuna makundi yanaichafua serikali ya awamu ya sita ionekane ufisadi umerudi na mambo yako ovyo, akisisitiza hatakubali na atasimamia haki za wananchi.

Mkuu wa Nchi alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akizindua gati katika Bandari ya Dar es Salaam, akionya: "Kuna makundi wanajua wanayoyafanya ndani ya serikali. Ni makundi hayo hayo yanageuka kusema serikali ya awamu ya sita ufisaidi umerudi, mambo yako ovyo, kumbe wao ndio wako ovyo.

"Na mambo yale hayakufanyika ndani ya awamu ya sita, yalifanyika huko nyuma, gari bovu linaangushiwa awamu ya sita. Sitakubali, sitakubali! Niliapa kusimamia haki za wananchi, nitasimama nao, nitasimama kutetea haki za wananchi, sitakubali!"

Katika utekelezaji wa ahadi yake hiyo kwa wananchi, Rais Samia alitangaza kuzivunja Bodi ya Mamlaka ya Badari Tanzania (TPA) na ile ya Shirika la Meli kwa kuwaondoa wenyeviti wake kutokana na kutoridhishwa na utendaji wao wa kazi. Rais Samia pia aliiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuchunguza dosari zilizojitokeza katika taarifa ya uchunguzi ya mifumo ya kielektroniki katika bandari ya Dar es Salaam na kuchukua hatua stahiki.

"TAKUKURU ninaagiza, ninatoa amri uchukue hatua dhidi ya watu hawa haraka na kama ripoti hii hamna, nitawapatia ya nini kilichofanyika hapa, watu waliofanya hayo wapo bado ofisini. Watu tunachekeana tu, tunatizamana tu.

"Watu wapo maofisini wanaendeleza wizi na ubadhirifu wa mali za umma, mifumo imekuwa ikichezewa, inaonyesha kuwa mizigo imelipiwa kutoka getini, lakini siyo kweli, haijalipiwa hivyo bandari kukosa mapato. Haya mapato yanayoonekana leo hayakupaswa kuwa hivyo yalivyo," alisema.

Alisema kumekuwa na dosari ya kuwapo mianya mingi ya upotevu wa mapato inayotokana na kukataa kwa makusudi kuweka mifumo madhubuti ya ukusanyaji mapato na mifumo inayosomana baina ya bandari na Mamlaka ya Mapato (TRA).

"Mapato katika Bandari ya Dar es Salaam yamekuwa yakipanda na kushuka na kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, bandari ilikusanya Sh. bilioni 901, mwaka 2020/21 ilikusanya Sh. bilioni 896 na matarajio ya 2021/22 ni kukusanya Sh. bilioni 980," alisema.

Rais alisema licha ya baadhi ya 'madudu' hayo kuonyeshwa kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), mpaka sasa hakuna hatua zilizochukuliwa na bado kuna mianya ya uvujaji wa mapato kutokana na mifumo ya malipo kuchezewa na wafanyakazi.

Alimkumbusha Mkurugenzi wa Bandari kuwa alimpeleka huko kusimamia na kudhibiti mapato ya mamlaka hiyo, akibainisha kuwa mambo yote yanatokea wakati Bodi ya Wakurugenzi wa Bandari ipo.

"Ipo kampuni iliingia mkataba wa Sh. milioni 694 na ililipwa Sh. milioni 600 lakini haikumaliza kazi iliyotakiwa na mkataba ukavunjwa, fedha zilikwenda bila kazi kufanywa, ripoti pia ilieleza kuwa utaratibu wa kutoa zabuni hizo haukufuatwa," alisema.

**WAZIRI KIKAANGONI**

Rais Samia alimtaka Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa kufanya marekebisho na kama hawezi amfuate wakae kikao cha pamoja na Katibu Mkuu Kiongozi kuona namna ya kufanya marekebisho kwenye wizara.

"Kasimamia kazi hii kama ninavyotarajia na utakaposhindwa njoo niambie 'dada nimeshindwa', nitaangalia mwingine ambaye labda ataweza kunisaidia lakini haya hayawezi kuendelea," Rais Samia alionya.

**WAHUJUMU MIUNDOMBINU**

Katika hatua nyingine, Rais Samia alisema jana kuwa licha ya serikali kutoa fedha nyingi kutekeleza miradi, wananchi wachache wasio na uzalendo wanaihujumu kwa kuiba vifaa na mafuta ya mitambo ya ujenzi.

Rais alitoa kauli hiyo wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi kwenye mradi wa ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka Mbagala wilayani Temeke, ambao ukikamilika utakuwa na watumiaji 673,800 kwa siku.

"Kuhujumu miradi hii siyo jambo jema, ninawaomba sana wananchi mtakapogundua kuna watu wana hujumu miradi hii, muwaseme, msiwaonee aibu, nikemee vitendo hivi visivyo na afya wala maslahi kwa taifa, raia wote tuwe walinzi wa miradi hii," aliagiza.

Rais Samia aliagiza zifanyike doria za mara kwa mara katika maeneo hayo ikiwa ni pamoja na hatua za kisheria zichukuliwe kwa wote watakaobainika kufanya vitendo vya kuhujumu miundombinu.

Pia aliitaka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Wakala wa Barabara (TANROADS) kuhakikisha kazi za ujenzi na ukarabati wa barabara na madaraja zinatekelezwa kwa viwango vilivyokusudiwa kimkataba ili zidumu kwa muda unaotarajiwa.

Rais Samia alisema siku hizi hata kama mradi umechelewa kisingizio ni UVIKO-19, akisisitiza kuwa licha ya mlipuko wa baa hilo kwenye mradi huo kulikuwa na uzembe wa makandarasi na watendaji wa serikali, akiagiza umalizike kwa muda uliopangwa.

"Mwezi Juni nilifanya ziara ndani ya wilaya ya Temeke, nikapita barabara ya mwendokasi, nikakuta ubovu ambao waziri umeutaja na nikaelekeza hatua zichukuliwe. Kwa ubovu ule kama viongozi wasingesimama na kusema hapa ni pabovu, mkandarasi angeendelea kutujengea kwa ubovu uleule," alionya.

## Shule yamshukuru Hayati Dk. Mengi

**Na Halfani Chusi**

SHULE ya Sekondari ya Wasichana John The Baptist High School, imemshukuru aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Hayati Dk. Reginald Mengi, kwa kuipatia Sh. milioni 100 kukamilisha miundombinu yake mbalimbali, yakiwamo mabweni.

Shukrani hizo zilitolewa jana jijini Dar es Salaam, na Mkuu wa shule hiyo, Roselina Mtambuka, wakati wa sherehe ya mahafali ya 14 ya kidato cha nne.

Alisema Hayati Dk. Mengi alipoalikwa katika mahafali ya mwaka 2010 alijionea jitihada za ujenzi wa shule zikiendelea ili kumuinua mwanamke, alivutiwa na kitendo hicho na kuhamasika kutoa Sh. milioni 100 taslimu ili kumalizia ujenzi wa sehemu zilizobakia.

"Kwa niaba ya bodi ya shule, napenda kumshukuru Hayati Dk. Mengi, alikuwa ni mtu mwenye maono ya mbali, alihamasika na alitufadhili pesa nyingi ili kukamilisha mradi huo, lakini pia niwashukuru wamiliki wa IPP na ITV Media" alisema na kuongeza:

"Tunamtakia pumziko la amani, ili kuendelea kumuenzi kama muasisi wa shule hii, tumeweza kuendeleza ujenzi wa kumalizia jengo la maabara ambalo tumeanza kujenga na kuendeleza ujenzi wa maghorofa pamoja na hosteli" alisema

Hata hivyo, Mtambuka alisema wanakabiliwa na changamoto ya ukumbi mkubwa kwa ajili ya shughuli za shule, sherehe na mikutano mbalimbali.

Aliwaomba baadhi ya wahitimu na wazazi wa watoto walioopita katika shule hiyo kuendelea kuiunga mkono katika mambo mbalimbali ili kuifanya iwe bora zaidi kitaaluma.

Mkurugenzi wa Radio One na Capital Radio, Deogratius Rweyunga, ambaye alimwakilisha mtoto wa Dk. Mengi, Abdiel Mengi, alisema amelichukua suala la ujenzi wa bwalo ambalo lilitajwa kama kikwazo na kuahidi kuliwakilisha kwa Abdiel.

"Kuondoka kwa Dk. Reginald Mengi, sio kufa kwa shule hii, kwa hiyo suala la bwalo la kulia chakula nimelichukua na nitaliwakilisha kwake, tutaangalia namna ya kufanya," alisema Rweyunga.

Rweyunga aliwataka wanafunzi waliohitimu kwenda kuwa watulivu kuwasaidia wazazi pamoja na kujiepusha na matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii, ambayo aliitaja ndio chachu ya mmomonyoyoko wa maadili kwa wanafunzi. Mwenyekiti wa Bodi ya Shule hiyo, Jalia Mayanja, aliwaomba wanafunzi wengine waliohitimu shule za msingi kutumia fursa hiyo kujiunga na shule hiyo kwa mwaka wa masomo 2022.

# Basi lilivyoteketea, kuua, kujeruhi 19

**Na Thobias Mwanakatwe**

MTU mmoja ambaye jina lake halijafahamika raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), amefariki dunia na wengine 19 kujeruhiwa baada ya basi la kampuni ya Classic kuyagonga malori mawili ya mizigo, likiwamo lililokuwa limeharibika kisha kuwaka moto.

Ajali hiyo imewasababishia hasara ya mamilioni ya fedha baadhi ya abiria kutokana na mali zao kuteketea.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Janeth Magomi, akizungumza na gazeti hili kwa simu, alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 4 usiku katika eneo la Mahenje, wilayani Mbozi.

Alisema basi hilo la abiria mali ya kampuni ya Classic lenye namba za usajili za DRC6884 AK 05 aina ya MAN Bus , lilikuwa likiendeshwa na Hamis Mazagila (33), raia wa Tanzania na lilikuwa likitokea jijini Dar es Salaam kuelekea katika mji wa Lubumbashi, DRC.

Alisema dereva wa basi hilo alikuwa mwendo kasi, hivyo kushindwa kulimudu na hatimaye kwenda kuligonga lori la mizigo T 242 DPR aina ya DAF lililokuwa limeharibika likiwa na shehena ya saruji likiwa njiani kuelekea Rukwa.

"Tumeambiwa chanzo cha ajali ni mwendo kasi kwani baada ya dereva wa basi kumshinda aliendа kulivaa lori lililoharibika likiwa na saruji ambaye alipoteza mwelekeo kabla ya kwenda kugongana lori lingine liliokuwa mbele yake likiwa na shehena ya mahindi likitokea Tunduma," alifafanua Kamanda Magomi.

Alilitaja lori lingine lililohusika katika ajali hiyo ni T 368 DSW aina ya DAF lililokuwa na shehena ya mahindi likitokea mjini Tunduma kwenda Mbeya.

**MAJERUHI**

Kamanda Magomi aliwataja majeruhi wa ajali hiyo ni Pitch Chasila (48), Sapwe Ulukale (37), Mbuyu Mwelele (43) wote raia wa DRC, pamoja na dereva wa basi Mazagila, ambao hali zao ni mbaya na wamehamishiwa Hospitali ya Rufami ya Kanda ya Mbeya kwa matibabu zaidi.

Wengine ambao wameendelea na matibabu katika Hospitali Teule ya Mkoa wa Songwe ni John Tarimo (53) ambaye ni dereva msaidizi wa basi, Fausta Matango (41), Marry Manyonga (42), Theo Chibanda (40), Ngoi Kakasi (42) wote raia wa DRC.

Majeruhi wengine ambao ni raia waDRC ni Katembelesa Mukonko (42), Ghisilaine Katesa (54), Fabian Kawongo (36), Chantel Numbi (31) na Kotemba Mozinga (46).

**MALI ZILIZOTEKETEA**

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, alisema katika ajali hiyo iliyosababisha basi hilo kuteketea kwa moto, hakuna mali iliyookolewa.

"Kama mlivyojionea wenyewe, tulifanikiwa kuudhibiti moto ule saa 11:00 alfajiri, lakini kutokana na kasi ya moto hatukuweza kuokoa kitu chochote," alisema.

Alisema jitihada za kujua thamani halisi ya hasara zinaendelea kwa kuwa basi hilo lilikuwa na mizigo ya biashara iliyokuwa ikipelekwa DRC.

Naye Mkurugenzi wa Hospitali Teule ya Mkoa wa Songwe, Dk. Lukombodzo Lulandala, alisema mbali na majeruhi wanne waliohamishiwa Hospitali ya Kanda Mbeya, majeruhi waliobaki hali zao zinaendelea vizuri.

Mmoja wa majeruhi, Marry Manyonga akizungumza na Nipashe akiwa Hospitali Teule ya Mkoa wa Songwe, alisema thamani ya mzigo wake ulioteketea kwa moto ni Dola za Marekani 7,000 sawa na zaidi ya shilingi milioni 16 za Tanzania.

Majeruhi mwingine, Rose Mukonko, alisema mzigo wake una thamani ya Dola za Marekani 3,000 sawa na shilingi milioni 7.



Mhasibu Mkuu wa Serikali, Leonard Mkude (kushoto), akikabidhi Tuzo ya Umahiri katika Uwasilishaji wa Taarifa za mahesabu kwa mwaka 2020 kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma, Rashid Mchatta, baada ya mkoa huo kuibuka mshindi wa kwanza, wakati wa hafla iliyoandaliwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA), Bunju, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Utekelezaji mradi wa shaba wanukia

**Mwandishi Wetu, Roma,** ITALIA

SHIRIKA la Taifa la Madini (STAMICO) limesaini mkataba wa makubaliano ya awali na Kampuni ya Suness Limited ya Italia kwa ajili ya kuendeleza mradi mkubwa wa shaba katika mkoa wa Kilimanjaro.

Suness Limited ni kampuni ya Kiitaliano inayojishughulisha na uchimbaji madini na kampuni hiyo imeonyesha utayari wa kushirikiana na STAMICO katika kuendeleza kwa pamoja mradi wa shaba.

Akizungumza baada ya kusaini mkataba huo, Mkurugenzi Mtendaji wa STAMICO, Dk. Venance Mwasse, amesema kuwa mkataba umesainiwa kupitia jukwaa la biashara na uwekezaji lililofanyika Roma Italia Alhamisi na Ijumaa.

Pamoja na mambo mengine, STAMICO ilielezea juu ya mradi mkubwa wa shaba unaopatikana katika mkoa wa Kilimanjaro ambapo pia mwekezaji alionyesha nia ya kuingia ubia na STAMICO.

"Shirika lina mradi wake mkubwa wa shaba mkoani Kilimanjaro wenye kiasi kikubwa cha mashapu ya shaba na kupitia jukwaa la wafanyabiashara na uwekezaji lililofanyika Roma Italia, tumewaeleza juu ya mradi huo na wenzetu wameonyesha kuvutiwa na mradi huo na tukakubaliana kusaini makubaliano ya awali na baadae watakuja Tanzania ili kwa pamoja twende kwenye eneo la mradi husika na mwishowe tuingie katika makubaliano ya pamoja ya kuendeleza mradi huo," alisema Dk.Mwasse.

Naye Rais wa Kampuni ya Sunless, Sandro Calo, alisema amefurahishwa na utiaji saini wa awali wa mkataba wa makubaliano kwa ajili ya kushirikiana na serikali ya Tanzania katika kuendeleza kwa pamoja mradi wa shaba.

"Nimefurahia kuanza kwa makubaliano haya mapya ambayo yataleta matokeo chanya kati ya nchi ya Tanzania na Italia na naahidi kuendeleza ushirikiano huu kwa maslahi mapana ya pande zote mbili katika sekta hii ya madini," alisema Calo. Utiaji saini wa makubaliano hayo ulishuhudiwa na Naibu Waziri, Wizara ya Madini, Prof. Shukrani Manya, Balozi wa Tanzania nchini Italia, Mahmoud Thabiti Kombo, Mkurugenzi Idara ya Diplomasia ya Uchumi katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Edwin Rutageruka na Mkurugenzi wa Kampuni ya Utalii ya Zanzibar Classic Safaris, Yussuf Salim Njama.

## UAMUZI MGUMU WAZIRI UMMY...

# Mbinu tisa za shule binafsi kushikilia watoto saa nyingi

**Na Christina Mwakangale**

BAADA ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Ummy Mwalimu kupiga marufuku wanafunzi kusoma saa za ziada siku na wakati wa likizo shuleni, Nipashe imebaini mbinu tisa zinazotumiwa na shule binafsi kufanikisha upotoshaji huo.

Ni marufuku aliyoitangaza waziri Jumanne wiki hii, akizingatia taarifa za athari kwa wanafunzi zilizotolewa na Chama cha Madaktari Tanzania (MAT) siku chache kabla, kikitangaza kuanza utafiti wa kiafya kwa watoto wanaokaa muda mrefu masomoni, pia kulazimishwa kubeba mizigo mizito ya vitabu.

Nipashe ambayo imekuwa ikifuatilia suala hilo kwa mwaka huu wote, imebaini namna shule binafsi zinavyowahadaa wazazi na uongozi wa kiserikali kusifahamike madhila hayo kwa watoto, lengo ni kufanikisha soko kupitia ufaulu, pia mapato zaidi kupitia ada.

Mbinu hizo zilizothibitishwa hata na baadhi ya walezi, zinajumuisha kuwahadaa kwenye mikutano ya wazazi; kuwahamishia wanafunzi bweni; ada kubwa kulipwa mwanzoni mwa mwaka; wanafunzi huhamia bwenini baada ya agizo la ada kutimizwa; kuwamiliki waratibu elimu kata na mtoto kudhibitiwa kutoa siri za bweni.

Zingine zinajumuisha; kutumia umaarufu wa shule kama hoja ya 'kuwateka' wazazi; Jumamosi na Jumapili wanafunzi hawavai sare ilhali wanaendelea na ratiba ya masomo kama siku zote na inapotokea mkasa, kinga yao kuu jumuiya za umoja wao kuja na utetezi wa pamoja.

Nipashe ilibaini shule ambazo wanafunzi wanakuwa masomoni kwa kati ya saa 12 hadi 14 kwa siku sita za wiki, huku baadhi yao zikiwamo za wilayani Ilala, zinaendesha ratiba hizo kwa siku zote za wiki.

Nipashe ilithibitishiwa na mzazi Simon (jina la pili tunalo) sambamba na mtumishi wa shule mojawapo (jina tunalo), akieleza hatua ya kwanza ni kwamba hoja huibuliwa kwenye mkutano wa wazazi shuleni kuhusu haja ya saa za ziada kwa watarajiwa wa mitihani ya taifa, ikiendana na darasa hilo lote lihamie bwenini.

Imegundulika baada ya ajenda hiyo kupita, mzazi Simon aliyejitambulisha kwa sura ya pili kwamba ni mwathirika wa mtoto wake, aliithibitishia Nipashe hatua inayofuata baada ya mkutano kuwa ni kuwatangazia rasmi wazazi nyongeza ya ada, sehemu kubwa (wastani asilimia 60) kulipwa mara moja baada ya watoto kuingia bwenini.



Waziri wa TAMISEMI, Ummy Mwalimu.

Kwa mujibu wa mzazi huyo, hoja ambayo gazeti hili iliibaini katika shule kadhaa, ni kwamba wakati wote mbinu kubwa ya kujinadi inayotumiwa na shule zinazofanya vizuri ni kuwa hiyo "ndiyo silaha ya ufanisi na ushindi".

Inaelezwa kuwa pindi tu wanafunzi wanapoingia katika maisha hayo mapya ya bwenini ndio unakuwa mwanzo wa madhila dhidi yao kwa madai wako hapo kwa baraka za wazazi, ikiendana na amri kali ya wasitoe siri ya maisha yao bwenini, pia ratiba za kuonana na wazazi hudhibitiwa.

Lingine lililogunduliwa kwenye uchunguzi huo, uongozi wa shule hujenga uhusiano wa karibu na ofisi ya mratibu elimu wa eneo lao ili kupata utetezi, jambo ambalo mzazi Simon alikiri kulishuhudia, hata kumpa mazingira ya kiulizo kwenye mkasa uliohusu msuguano wake na shule kuhusu alichokiita uonevu kwa mwanawe katika shule ya jijini Dar es Salaam.

Mbinu nyingine iliyobainika ni kwamba ili kuficha siri na ratiba ya maisha ya wanafunzi walio bwenini na hata wachache kuwa nje ya bweni, kwa siku za wikiendi (Jumamosi na Jumapili) hawavai sare, ila ratiba zao za masomo zinabaki vilevile.

Nipashe katika uchunguzi wake ililazimika kuuhoji uongozi wa mamlaka husika inayosimamia shule binafsi nchini mapema mwaka huu na iliitolea ufafanuzi unaokinzana na maelekezo ya sera ya elimu inayotumika nchini.

**SERA ELIMU INASEMAJE?**

Sera ya Elimu ya Msingi Toleo la Tatu la Mwaka 2019 inaelekeza mwanafunzi akae darasani kwa siku tano za wiki, ikiwa na jumla ya muda usiozidi saa 30, ikifafanua: "Mwaka wa masomo utakuwa na siku 194 ambazo ni sawa na wiki 39 kwa Darasa la III-VI.

"Darasa la VII watakuwa na wiki 34 kutokana na darasa hilo kuwa na mtihani wa mwisho mwezi Septemba kila mwaka.

"Mwaka umegawanywa katika mihula miwili ya masomo. Kila muhula utakuwa na wiki mbili zitakazotumika kwa mitihani. Muda wa kusoma utakuwa ni saa sita kwa siku kwa Darasa la III-VII. Muda wa kipindi ni dakika 40. Kutakuwa na vipindi vinane kwa siku kwa wanafunzi wote isipokuwa siku ya Ijumaa ambayo itakuwa na vipindi sita."

Kwa mujibu wa sera hiyo, wanafunzi watasoma vipindi 38 kwa wiki, ambayo ni sawa na jumla dakika 1,520 ambayo ni sawa na saa 25 na dakika 33; hiyo inaangukia wastani wa saa tano kwa kila siku ya masomo, uwiano unaoonyesha wastani wa saa sita uliotajwa kwenye sera, unajumuisha muda wa ziada wa mengineyo kama mapumziko.

**USHUHUDA WA MWANAFUNZI**

Mwanafunzi (jina tunalo) mhitimu wa darasa la saba, kutoka shule ya mkoani Dar es Salaam, aliiambia Nipashe kuwa wote walio darasa la saba waliishi bwenini kwa ratiba ya saa 14 masomoni kati ya saa 12 asubuhi na saa nne usiku kwa siku za Jumatatu hadi Jumamosi.

Kwenye ratiba hiyo yenye ziada ya saa nane kila siku masomoni ikiwamo Jumamosi ikilinganishwa na maelekezo ya sera, alisema Jumapili ratiba yao ilianzia kwenye ibada saa tatu asubuhi na baada kula mchana, waliingia masomoni ratiba ikiisha kati ya saa mbili na saa nne usiku.

Akianisha mpangilio wa ratiba hiyo kila siku iliyowashurutishwa mara nyingi kufua nguo zao usiku baada ya kutoka darasani, waliamshwa saa 10 alfajiri kujiandaa kisha kupelekwa na gari la shule hadi wanakosoma kutoka mbali wanakolala, lakini dada zao waliishi jirani na madarasa.

Huku akikumbuka maisha ya uchovu alioupata, alisema masomo yalianza rasmi saa 12 asubuhi baada ya kupata kifungua kinywa cha uji, kisha kifungua kinywa kingine katika mapumziko ya nusu saa nne asubuhi, kisha mchana saa saba walipumzika kwa saa moja ya mlo ya kurudi darasani.

Alisimulia kuwa saa 11 jioni walipumzika nusu saa wakinywa uji na kurudi darasani hadi saa mbili usiku na baada ya nusu saa walirudi tena darasani hadi saa nne usiku kukamilisha ratiba ambayo hata wenzao wachache walioishi nyumbani kutokana na hitilafu za kiafya, wazazi wao walilazimika kuwafuata.

**USHUHUDA WA MZAZI**

Mzazi Simon anasimulia namna alivyogundua kuwapo jambo nyuma ya pazia kupitia kikao cha wazazi shuleni, pale alipoanza kulazimishwa mtoto wake mwenye hitilafu kiafya akae bwenini, pia kushindwa kupewa uthibitisho wa kisheria unaoendana na ratiba hiyo yenye ziada nyingi hasi ambazo hazikuanishwa kwenye mkutano wa wazazi. Alikuwa tayari alishalipa ada. Aliieleza Nipashe kushangazwa na Mratibu wa Elimu wa eneo hilo (jina tunalo) namna ushirikiano na uamuzi wa jambo hilo ilivyoelemea upande mmoja, huku akitetea ratiba hiyo ni uamuzi wa wazazi shuleni, naye anauheshimu.

Simon alisema hata pale alipohoji nafasi ya Sera ya Elimu ambayo ndio mwongozo mkuu katika kufafanua jambo hilo kwenye kikao cha pamoja, bado mratibu huyo hakutoa ushirikiano wa ufafanuzi wake huku mamlaka ya shule ikitamtakia "hiyo sera ni kwa ajili ya shule za serikali."

Kwa mujibu wa mzazi huyo, awali uongozi wa shule haukuwa tayari kumrejeshea ada ya mwanawe aliyekuwa na shida kiafya, lakini alishangaa miezi kadhaa baadaye aliombwa kama anaweza amhamishe mtoto pasipo ada kurejeshwa, jambo alilolikataa na kuliwasilisha kisheria katika ngazi ya halmashauri walikotatua mara moja baada ya Mratibu Elimu kushindwa.

Awali Nipashe ikifuatilia suala hilo lililoonekana kumea kwenye shule kadhaa za Dar es Salaam na kumdadisi Katibu Umoja wa Wamiliki na Mameneja wa Shule na Vyuo visivyokuwa vya kiserikali (TAMONGSCO), Benjamin Nkonya, aliyekiri kuwapo ratiba ya ziada shuleni akitaja sababu kubwa ni kufidia muda wa ziada kutokana na shule kufungwa miezi kadhaa dhidi ya corona.

HABARI KITAIFA

# Wasichana wang'ara tuzo za mwanafunzi bora ARU

**Na Joseph Mwendapole**

KWA mwaka wa tatu mfululizo wanafunzi wa kike wamewapiku wenzao wa kiume na kuongoza kwa kutwaa tuzo nyingi za wanafunzi bora katika Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU).

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Gabriel Kassenga wakati wa hafla ya utoaji wa tuzo kwa wanafunzi waliofanya vizuri kwenye masomo yao kabla ya mahafali ya chuo hicho.

Jumla ya tuzo 135 zilitolewa kwenye hafla hiyo na kati ya tuzo hizo, 74 ambazo ni wastani wa asilimia 54.8 ya zawadi zote zimechukuliwa na wasichana na 61 ambazo ni asilimia 45.2 zimechukuliwa na wavulana.

Alisema ingawa idadi ya wasichana chuoni hapo ni asilimia 40, lakini wamekuwa wakifanya vizuri na kutwaa tuzo hali ambayo inadhihirisha kwamba wanawake wana uwezo wa kufanya vyema kwenye masomo ya sayansi kinyume na fikra za baadhi ya watu.

"Katika ushindi wa jumla wanafunzi wawili wamefungana kwa alama ambao ni msichana na mvulana hivyo utaona kwamba wasichana wamepata tuzo nyingi kuliko wavulana ingawa kwa idadi wasichana ni wachache hapa chuoni kulinganisha na idadi ya wavulana," alisema.

Aliwapongeza wanafunzi wote waliopokea tuzo hizo na kuwasihi waendelee kusoma kwa bidii ili waje kuwa mfano wa kuigwa na wanafunzi wenzao na jamii kwa ujumla.

"Ninapenda kuwapongeza wanafunzi wahitimu kwa kujinyakulia tuzo mbalimbali na wengine wamekuwa wakitwaa tuzo kama hizi kwa miaka yote wakiwa chuoni hapa hii ina maana kwamba kwenye juhudi ya kweli mafanikio hupatikana," alisema.

Aliongeza kuwa sherehe hizo ambazo hufanyika kila mwaka ni muhimu kwani hutoa hamasa kwa wanafunzi wa chuo hicho ili waendelee kuweka juhudi kwenye masomo na hatimaye waweze kupata ufaulu wa juu.

Prof. Kassenga alisema sherehe hizo zimekuwa zikiwezeshwa na wadau mbalimbali kwa kujitolea ufadhili wa hali na mali kwa wanafunzi waliofuzu kupata tuzo hizo na aliwaomba wasichoke kuwasaidia kufadhili tuzo hizo.

Alisema zawadi mbalimbali zinazotolewa na wafadhili hao zimekuwa zikiwasaidia wanafunzi hao kuongeza mitaji na utendaji kazi mara wanapomaliza masomo yao.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo (wa tatu kulia), akiwa katika ziara ya kikazi ya kukagua uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira katika mgodi wa kati wa dhahabu wa Taichangxin, wilayani Geita juzi. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Sinyamule. **PICHA: OMR**

# Utiririshaji maji yenye sumu wamshtua waziri

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, ameelekeza wamiliki wa migodi midogo na ya kati inayotumia zebaki na cyanide katika uchenjuaji, waache kutiririsha ovyo maji yenye sumu na badala yake wafuate taratibu za kimazingira ili kulinda maisha ya wananchi.

Jafo alitoa jana maelekezo hayo alipofanya ziara katika mgodi wa kati wa Taichangxin ulioko katika mkoa wa Geita na kutoa siku 90 kwa uongozi wa mgodi huo kuzifanyia kazi dosari za kimazingira zilizobainika.

Alisema kuwa hajaridhishwa na namna mgodi huo unavyoendeshwa kwa kushindwa kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa mazingira ikiwamo kujenga na kutumia shimo la takasumu bila kupata cheti cha tathmini ya athari kwa mazingira na kuacha maji yenye sumu kutiririka ovyo.

Waziri Jafo pia alielekeza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Ziwa kuchukua hatua stahiki kwa uongozi wa mgodi huo kwa mujibu wa sheria.

"Mgodi huu unahatarisha maisha ya watu japo ninafahamu unaleta fedha kwa serikali na kutoa ajira, lakini ninyi wawekezaji hamtendi haki kwa wananchi wa kawaida na ukiangalia mazao yanalimwa kule bondeni kama kuna 'heavy metals' (kemikali) maana yake inakwenda kuathiri afya za wananchi.

"Watu wangu (NEMC) walitoa maelekezo mrekebishe hizi changamoto za kimazingira tangu tarehe tano mwezi wa nane (Agosti) maana yeke tarehe tano mwezi wa kumi na moja (Novemba) mlitakiwa muwe mmerekebisha lakini bahati mbaya mpaka leo hii marekebisho hakuna, mnafanya kosa juu ya kosa," alionya.

Meneja wa Kanda ya Ziwa wa NEMC, Jarome Kayombo, alisema wamepokea maelekezo ya waziri na kuahidi kuchukua sampuli za maji yanayotiririka ili kubaini ni kwa kiasi gani uchafuzi huo unafanyika.

Alisema baada ya kubaini upungufu huo waliwapa onyo kwa kuwapiga faini lakini hadi Novemba hawajatekeleza, hivyo watashauriana na mwanasheria wa baraza kuona hatua za kuchukua dhidi ya mwekezaji huyo.

Aliongeza kuwa wataendelea kushirikiana na wawekezaji wakiwamo wenye migodi ya dhahabu kwa kutoa ushauri wa kitaalamu kimazingira kwa kuwa NEMC haiko kwa ajili ya kutoa adhabu tu, bali pia kuwasaidia ili wafuate sheria.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Rosemary Sinyamule, aliomba NEMC kuwashirikisha katika shughuli za ukaguzi wa migodi ikiwamo kuwapatia ripoti ili wawe wanafuatilia maelekezo endapo yanatekelezwa ama la.

Alisema uongozi wa mkoa utaendelea kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais katika kuhakikisha maelekezo ya serikali kuhusu mazingira yanatekelezwa ili kulinda afya za wananchi.

Mtaalamu wa Mazingira wa Mgodi huo, Francis Sirili, aliahidi kuwa watafuata maelekezo yaliyotolewa na serikali kwa kuzifanyia kazi dosari zilizobainishwa.

# Halmashauri yapatiwa mkopo kupima viwanja

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro inatarajia kutekeleza mradi wa kupanga, kupima na kumilikisha viwanja eneo la ekari 4,500 baada ya kumalizika mgogoro kati ya wawekezaji wa Star City wa shamba la Tungi na hivyo kupatiwa mkopo wa Sh. bilioni 1.128 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro, Ally Machela alibainisha hayo juzi kwenye mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani uliofanyika ukumbi wa Soko Kuu la Chifu Kingalu la Morogoro chini ya Meya Pascal Kihanga.

Machela alisema kuwa mara baada ya kupatiwa ekari hizo, halmashauri ya Manispaa katika vyanzo vyake vya kawaida ilikuwa haina bajeti ya mpango huo, hivyo iliandika andiko na kuliwasilisha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Mendeleo ya Makazi kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na Hazina.

"Tumefanikiwa kupatiwa mkopo wa Sh. bilioni 1.128, hivyo kwa mujibu wa sheria na kanuni pamoja na kwamba shughuli zote za Manispaa na baraza la madiwani zimekasimiwa na kamati ya fedha lakini katika kipengele cha mkopo wenye mamlaka ya kupitisha ni baraza," alisema Machela.

Aliongeza kuwa katika mpango huo, vinatarajiwa kupatikana viwanja 6,250 kutoka ekari 4,500 ambazo zimerudishwa kwa wananchi na wawekezaji wa Star City eneo la Tungi Estate na utekelezaji wake, manispaa itapata asilimia 45 ya viwanja vitakavyozalishwa na asilimia 55 itabaki kwa wananchi wa eneo la Star City.

"Tumepata eneo hili baada ya kutatua mgogoro wa ardhi kati ya manispaa na Star City na wananchi na kupata ekari 4,500 na katika ekari hizo, tuna mkataba na wananchi ambao wanahodhi eneo hilo kwa mujibu wa makubaliano ya ule mkataba. Pale wananchi watapata asilimia 55 na manispaa itapata asilimia 45," alisema.

Mbali na hilo, alisema kuwa kwa mwaka wa fedha 2021/22, manispaa ilitenga bajeti ya Sh. milioni 127 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za kupanga na kupima maeneo lakini kiwango hicho kilikuwa pungufu kwa Sh. bilioni 1.031.

Baadhi ya madiwani wa baraza licha ya kuridhia mkopo huo, walitoa agalizo kwa watendaji wa halmashauri ambao ni wasimamizi wa mpango huo kuwa makini na kuhakikisha fedha zinatumika kwa malengo ya yaliyokusudiwa na si vinginevyo kwa vile hizo ni kodi za wananchi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ma-RC, ma-DC libebeni jukumu chanjo corona

**TANZANIA** imeendelea kuchukua hatua dhidi ya ugonjwa hatari wa Uviko-19 kwa kuwapa jukumu wakuu wa mikoa na wilaya kuhusu suala la chanjo.

Pamoja na kuwahimiza, kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizi hayo, ambayo yameshaua watu zaidi ya 700 na wengine zaidi kuugua, sasa serikali imeelekeza nguvu katika suala la kuelimisha, kuhamasisha na kuwashawishi kuchanja.

Hatua ya kuhamasisha na kuelimisha wananchi kuchanja inatokana na nchi yetu kuruhusu chanjo, hivyo kufunguliwa milango mataifa mbalimbali na washirika wengine wa maendeleo kuleta aina mbalimbali za chanjo nchini ili wananchi wengi wachanje.

Katika mwendelezo wa nchi marafiki na washirika wa maendeleo kuisaidia nchi yetu kukabiliana na janga hilo, juzi Tanzania ilipokea dozi ya chanjo 115,200 aina ya Johnson & Johnson kutoka Ubelgiji kupitia mpango wa Covax Facility. Hiyo ni mara ya kwanza Tanzania kupokea dozi ya UVIKO-19 kutoka Ubelgiji baada ya zile za kutoka Marekani na China.

Akipokea msaada huo kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, aliwaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kwenda kwenye jamii na kushiriki kampeni za kuongeza uelewa ili kasi ya watu kuchanja iongezeke.

Aliwataka viongozi hao wahakikishe asilimia 60 ya Watanzania wanachanjwa na mpaka sasa serikali imepokea dozi 4,421,540 zikihusisha chanjo za Sinopharm, Pfizer na Johnson & Johnson.

Tunaishukuru Ubelgiji kwa msaada huo ambao unadhihirisha kuwa ni rafiki na mshirika wetu wa dhati katika maendeleo, na hii inadhihirisha msemo kwamba 'rafiki wakati wa shida ni rafiki wa kweli'. Tunawasisitiza Watanzania kubadili fikra kwa kukubali kwa dhati na kwenda kuchanja kwa ajili ya maisha yao na ya wengine. Tunaendelea kutoa msisitizo wa umuhimu wa chanjo hii kutokana na mwitikio mdogo wa kuchanja tangu kuzinduliwa kwa chanjo Agosti mwaka huu, licha la janga la ugonjwa huo kuendelea kuwa tishio duniani.

Tunakubaliana kwa dhati na maelekezo ya Waziri Gwajima kwa wakuu wa mikoa na wilaya kutoka ofisini kwenda kuongoza kampeni ya elimu kwa jamii kwa lengo la kuongeza uelewa kuhusu umuhimu wa chanjo.

Tunawashauri viongozi hao wakuu wa mikoa na wilaya kuyapokea maelekezo hayo kwa mwitikio chanya tukiamini kuwa kwa kuwa wana ushawishi katika maeneo yao ya utawala wataongeza nguvu katika kampeni ya kutoa elimu kwa umma.

Tunaamini kuwa Uviko-19 ni vita ya taifa, hivyo wakuu wa mikoa na wilaya watatumia muda wao na nguvu zo ziada katika kulisimamia hili, bila kusita kuwaeleza wananchi kwamba kujitokeza kuchanja kwa sasa kuna umuhimu mkubwa, kutokana na taarifa za kulipuka kwa wimbi la nne.

Tahadhari kuhusu wimbi la gonjwa hili ilitolewa Alhamisi na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alipokuwa anazindua maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru wa Tanzania Bara na kurudiwa tena jana na Rais Samia Suluhu Hassan, huku wakiwataka wananchi kuchukua tahadhari zinazoelekezwa na wataalamu wa afya.

Ni matarajio yetu kuwa nguvu ya wakuu wa mikoa na wilaya itaongeza kasi ambayo imeshaonyeshwa na wataalamu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika kuongeza idadi ya wananchi wanaopata chanjo.

Tunaona kwamba viongozi hawa wakipimwa mafanikio yao kwa kigezo cha chanjo katika utekelezaji wa majukumu yao, itasaidia kubainisha ni viongozi wapi wanafaa kuendelea kushikilia nafasi hizo. Bila shaka wizara husika itakuwa ikitoa takwimu kuonyesha matokeo ya chanjo ngazi ya mikoa na wilaya zake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

### Kulinda uhuru, inawezekana kila mmoja akitimiza wajibu

Na Sabato Kasika

**DESEMBA** 9 mwaka huu, Watanzania watakuwa wanahitimisha kilele cha maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru wa nchi yao, ambao ulipatikana kwa wakoloni, Desemba 9 mwaka 1961, wakati huo ikiitwa Tanganyika.

Tangu mwaka 1964 jina Tanganyika lilifutika baada ya kuungana na Zanzibar na kuzaliwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na nchi imeendelea kuwa ya amani, umoja na mshikamano.

Miaka 60 ya uhuru huku watu wakiendelea kuishi kwa amani umoja na mshikamano, ni jambo la kujivunia, hasa kutokana na ukweli kwamba, baadhi ya nchi zikiwamo za jirani na Tanzania hazina amani.

Hali hiyo imefanya Tanzania kuwa kimbilio la wageni wanaokimbia kutoka katika nchi zao kuepuka vita vya wenyewe ambavyo husababishwa na ukosefu wa amani, umoja na mshikamano.

Amani, umoja na mshikamano vilivyopo nchini, ni matokeo ya Watanzania kila mmoja kutimiza wajibu wake wa kuzingatia misingi na utamaduni ulioanza mara tu baada ya nchi kupata uhuru.

Huo ndiyo msingi wa maendeleo, kwani bila amani, umoja na mshikamano, ni vigumu watu kwenda kwenye shughuli za uzalishaji mali, hivyo kama Watanzania, hatunabudi kujipongeza kwa kulinda tunu hiyo.

Viongozi walioshiriki kuleta uhuru wa nchi hii na hata muungano wa Tanganyika na Zanzibar, baadhi yao wameshatangulia mbele ya haki, wakiwa wameiacha nchi ikiwa salama hadi sasa.

Hiyo inatokana na kutambua kwamba, amani, umoja na mshikamano ni nyenzo muhimu, ambayo inasaidia kulifanya taifa kuwa imara bila watu wake kubaguana kwa rangi, dini wala kabila.

Miongoni mwa viongozi hao ni Mwalimu Julius Nyerere na Abeid Aman Karume, ambao waliamua kuunganisha Tanganyika na Zanzibar na kuzaliwa Tanzania. Wote hao wameshatangulia mbele ya haki.

Wameacha misingi imara ambayo nchi imekuwa ikiendelea kuitumia ikiwamo kupokezana kijiti cha uongozi wa juu bila tatizo, hali ambayo pia ni ya kujivunia kutokana na misingi iliyoasisiwa na viongozi hao.

Wakati huu tunapoelekea kwenye kilele cha maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru, ni muhimu kukumbuka hilo, lakini pia msemo huu wa Mwalimu Nyerere kwamba; 'Inawezekana Timiza wajibu wako'.

Hata kwenye suala la amani, umoja na mshikamano, inawezekana, hivyo kila mmoja aendelee kutimiza wajibu wake kwa kuepuka chokochoko ambazo zinaweza kusababisha Watanzania wakahasimiana.

Viongozi waasisi na Watanzania wengine ambao majina yao hayakuingizwa kwenye historia walipambana hadi ikawezekana Tanganyika kuwa uhuru, na sasa kilichobaki, ni sisi kutambua kwamba inawezekana kuendelea kuulinda uhuru huo ambao sasa unatimiza miaka 60.

Kinachotakiwa ni kutimiza wajibu, iwe nyumbani, sehemu ya kazi au mahali popote, lengo likiwa ni kwa ajili ya maendeleo yake na nchi kwa ujumla, ambayo bila amani, umoja na mshikamano hayawezi kuwapo.

Kimsingi, Mwalimu Nyerere alikuwa na misemo mingi iliyotumika kwa namna mbalimbali ikiwamo kuonya, kukosoa, kukemea uovu, kuasa jamii juu ya uasi, ili Watanzania waendelee kuwa wamoja.

Si vibaya kusema kwamba, miaka 60 ya uhuru Watanzania wamethubutu kuwa na amani, umoja na mshikamano wameweza, kilichobaki sasa ni kuendelea kuilinda kadri inavyowezekana.

Hilo lifanyike kwa kutambua kuwa amani, umoja na mshikamano, ni nyenzo ya msingi katika mchakato wa maendeleo fungamani ya binadamu, kwani kinyume cha hapo ni migogoro, vita na mipasuko ya kijamii.

Amani, umoja na mshikamano ni vya msingi ambavyo viongozi wa zamani walijitoa muhanga kwa ajili ya kuhakikisha taifa lao linakuwa na watu ambao ni wamoja na wakafanikiwa katika hilo.

Pamoja na jitihada mbalimbali ambazo zimekuwa zikifanyika kutunza amani na kuendeleza mshikamano na umoja wa kitaifa kwa miaka 60 tangu uhuru, Watanzania tunapaswa kuelewa kuwa dunia hubadilika kulingana na wakati.

Lazima kujipima kwa kufanya tafakuri ya kina ya mahitaji ya sasa hasa kwa kuzingatia kuwa jamii yetu ina kizazi kipya. Kwa msingi huo, ni wakati wa kuangalia sheria zetu, mifumo na mambo mengine kama yanakidhi mahitaji ya sasa na matarajio ya Watanzania wengi.

Ikiwezekana hata Katiba yetu, ambayo ni sheria mama iangaliwe kwa kufanyiwa maboresho yanayoendana na matakwa ya sasa, ili amani, mshikamano na umoja wa kitaifa viendelee kuwapo.

**SAFU/MAKALA**

**KWA MASLAHI YA TAIFA**

# Asante Rais Samia kwa 'nonsense' ya sukari



**Na Pascal Mayalla**

NAOMBA kuanza mada yangu ya leo, kwa kufundisha lugha kidogo, neno "nonsense" ni neno la kizungu lenye kumaanisha "ujinga", hivyo uamuzi wowote unaoitwa "nonsense" ni "uamuzi wa kijinga", Baba wa Taifa, alilitumia sana neno hili "nonsense", ila yeye Baba wa Taifa, hakuishia tu kwenye kulaumu maamuzi ya kijinga, "nonsense", bali pia aliwaita watoa maamuzi hayo "wajinga", ninayo mifano mingi ya Mwalimu Nyerere kutumia neno "nonsense".

Mfano mzuri ni wakati Mwalimu Nyerere anaaga na kungatuka kwenye urais, alikiri serikali yake imefanya makosa mengi tuu , akakiri kuna baadhi ya maamuzi yalikuwa ni "nonsense", makosa, lakini pia akasema "kufanya kosa si kosa, kosa kurudia kosa".

Wakati tukijiandaa kwa uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi, ile 1995, Mwalimu alizungumza na sisi waandishi wa habari, kwenye ukumbi wa Hoteli ya Kilimanjaro, na mimi nilikuwepo, akizungungumzia ubinafsishaji wa benki ya NBC, Mwalimu akaishangaa serikali kukubali masharti ya nchi mabeberu, kuwa NBC ni li benki likubwa sana, lenye nguvu sana, lazima livunjwe, ndipo turuhusu ushindani wa mabenki, Mwalimu akauliza NBC ina ukubwa gani?, "a mere NBC?!, this is "nonsense".

Ninayo mifano mingi ya neno "nonsense" toka kwa Mwalimu.

Mtu kuambiwa mjinga, ni kweli umetukanwa lakini ujinga siyo tusi, ni kutojua tu, mtu mjinga akiisha elimishwa, ujinga unamtoka, anakuwa mwerevu. Mtu mjinga akiisha elimishwa, ujinga usipomtoka, huyo sasa sio mjinga, huyo ni mpumbavu!. Rais Mkapa wakati wa uzinduzi wa kampeni za CCM kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, aliwaita watu fulani "malofa na wapumbavu", na haikuwa habari kubwa, Rais Magufuli, aliwahi kumuita waziri fulani "mpumbavu" na haikuwa habari kubwa.

Juzi kati katika ziara za Rais Yoweri Museveni Tanzania, katika kuzungumzia hoja ya sukari, Rais Samia pia kalitumia neno "nonsense". Baada ya kutumika kwa neno hilo, huku kwenye mitandao ya kijamii kukalipuka "Rais Samia katukana", aliyetoa msimamo kuwa Tanzania hatutanunua sukari ya Uganda ni Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda. Baadhi ya mitandao ya kijamii ikamchagiza Prof. Mkenda kuwa asikubali kutukanwa hadharani, bora ajiuzulu kutunza heshima yake na asipojiuzulu atatumbuliwa!.

Siyo mara moja nimeongea katika makala zangu, kuwa media ya Tanzania, hatuna watu wazuri wa kufanya uchambuzi wa habari, "news analysis", Rais Samia alipotumia neno "Nonsense", hakumtukana Waziri Prof. Mkenda ni "nonsense", ameshangaa uamuzi ule wa kugomea sukari ya Uganda kwa kisingizio cha kulinda viwanda vya ndani, hivyo lile neno "nonsense" ni neno kwa ajili ya uamuzi ule na sio kwa ajili ya kumlenga mtu Prof. Mkenda.

Naomba tukubaliane, kama neno "nonsense" ni kwa uamuzi ule wa kugomea kuagiza sukari kutoka nchini Uganda, au uamuzi wa kugomea kuagiza bidhaa zozote kwa nia njema na lengo zuri la kulinda viwanda vya ndani, uamuzi kuhusu sukari, haukutolewa na Waziri Prof. Mkenda kusema ni uamuzi wake binafsi, pia nilimsikia Waziri Mkuu, Majaliwa Kassim Majaliwa akiuzungumzia. Huu ni uamuzi wa Baraza la Mawaziri lililopita, hivyo kauli ya Rais Samia haimlengi mtu, inalenga uamuzi wa kugomea kuagiza sukari ya jirani Uganda.

Sasa twende kwenye ukweli wenyewe wa alichokisema Rais Samia uamuzi ule kweli ni "nonsense". Hii maana yake ni kile niliwahi kukisema katika makala zangu za nyuma, kuwa viongozi wetu sio malaika, ni binadamu, hivyo wanaweza kabisa kufanya makosa na kutoa uamuzi "nonsense", kama bazara la mawaziri limeweza kupitisha uamuzi kama huo, hili la sukari ni uthibitisho tu wa uwezokano serikali yetu kufanya maamuzi "nonsense".

Tena nonsense kubwa kuliko ya sukari, siyo kwa serikali yetu kugomea kuingiza nchini sukari ya jirani zetu wa Uganda, serikali yetu iligomea kuingiza Tanzania Bara sukari kutoka Zanzibar!. Wakati huku bara tuna uhaba wa sukari, sukari ilipanda bei kutoka shilingi 1,800 kwa kilo, hadi shilingi 2,500 kwa kilo. Kule Zanzibar bei ilibaki 1,500 hadi 2,000.

Kiwanda cha sukari Zanzibar, kilikuwa na sukari ya kutosheleza kabisa kumaliza upungufu wa sukari huku bara, hivyo kikaomba kuleta sukari yake Bara kukabili upungufu, haswa kwa kuzingatia bei ya huku Bara kuwa imechangamka kuliko bei ya Zanzibar, ilikataliwa.

Waziri wa Viwanda na Biashara wa Zanzibar, Amina Salum Ali, akavuka bahari, kuja bara kusemezana na waziri mwenzake...lakini wapi, alikataliwa!. Waziri Amina Salum Ali akaigeukia taasisi ya TradeMark East Afrika inayoshughulika na kuondoa vikwazo vya kibiashara visivyo vya kikodi (non tariff barriers), na kukiripoti hicho kikwazo cha sukari.

Yaani Tanzania bara inakabiliwa na uhaba wa sukari, Zanzibar inayo sukari ya ziada bwelele, Zanzibar inakataliwa kuingiza sukari yake bara, na badala yake, wenye viwanda ndio wanaoruhusiwa kuagiza sukari ya bei chee kutoka ng'ambo, kufidia huo upunguful, kwa uamuzi kama huu, ni neno gani zuri zaidi ya kulitumia zaidi ya neno "nonsense?".

Nampongeza sana rais Samia kwa kukemea na kukomesha hii nonsense ya kwenye sukari, na sasa nitoe wito kwa rais wetu Mama Samia, hizi nonsense za kwenye sukari, zisiishie tu kwenye sukari, twende na kwenye nonsense nyingine zote za uondoshaji wa vikwazo vya uingizaji nchini bidhaa muhimu ambazo viwanda vya ndani vimeshindwa kutosheleza mahitaji ya bidhaa hizo.

Kwa sasa taifa linakabiliwa na upungufu wa sementi, mfuko wa sementi ya Tanzania kwa mikoa ya pembezoni, kama Arusha, na Moshi, imefikia bei ya shilingi 24,000 kwa mfuko. Sementi ya Kenya ni shilingi 12,000 kwa mfuko mpaka inafika dukani Tanzania. Watu wanahitaji sementi haipo, hapo kwa jirani yetu sementi bwelele, bei chee, lakini hairuhusiwi kuingia Tanzania, kwa lengo la kulinda viwanda vya ndani. Hii pia ni nonsense!. Hivyo baada ya hii nonsense ya sukari, twende kwenye nonse nyingine zote za vikwazo vya uingizaji bidhaa.

Angalizo: Kuunga mkono huu msimamo wa rais Samia kuondoa nonsense ya sukari, na kutaka nonsense nyingine zote ziondoshwe, namaanisha kufungua milango ya soko huria kwa zile bidhaa tu za muhimu ambazo viwanda vyetu vya ndani, vimeshindwa kuzalisha kukidhi mahitaji ya kutosheleza soko la ndani, na sio soko holela. Viwanda vya ndani vikifanikiwa kuzalisha kutosheleza soko, tuendelee kuvilinda, hata kama ulinzi huo utatuumiza sisi wananchi kulazimika kununua bidhaa zote zinazozalishwa nchini kwa bei kubwa, ndiko kujenga nchi kwenyewe na sio kukimbilia cheap imports kwasababu tu ni cheap!.

Wasalaam.

**Paskali.Pascal Mayalla**
**Mob. +255 754 270403**

---

## MIAKA MIWILI KIFO CHA FARU FAUSTA:

# Kazi kubwa imefanyika kudhibiti ujangili

**Na Sanula Athanas**

NI vigumu kuuzungumzia uchumi wa Tanzania pasi na kuutaja utalii. Sekta hiyo sasa inachangia robo ya fedha za kigeni na asilimia 17.5 ya pato la taifa.

Kadri unavyozama kuuchambua utalii huo, unakutana na makundi makuu ya wanyamapori ambao ndiyo vivutio vinavyosafirisha wageni kutoka mbali kuja nchini kuwashuhudia.

Hapo unabaini kuna wanyama wakubwa watano ambao ni tembo, faru, twiga, nyati na simba.

Unapodokeza mnyama faru, hapo ndipo shida inaposikika. Kwa nini? Wanyama hao ambao wamekuwa kivutio kikuu cha watalii, katika miaka ya karibuni walitajwa kuwa katika hatari ya kutoweka kisi cha kutikisa mwelekeo wa taifa.

Wakati kuna mtazamo wa jumla, katika mustakabali wa kipekee, Novemba 27 mwaka huu ilikuwa siku maalum kwa wadau wote wa wanyamapori na washirika wa sekta ya utalii, kwa maana ya kumbukumbu ya miaka miwili kamili tangu kifo cha faru Fausta. Huyu ni aliyekuwa faru mzee zaidi si tu kwa Tanzania, bali pia dunia nzima, akishikilia rekodi hiyo.

Faru Fausta alikufa Novemba 27, 2019 kwenye Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro akiwa na umri wa miaka 57.Mnyama huyo alishika hadhi ya kitaifa, kwa kuwa mwaka 2017 suala la matunzo yake lilifikia hatua ya kuibua mjadala kisiasa ndani ya Bunge, mada kuu katika hoja zote zilibeba mtazamo wa msimamo wa maslahi yake.

Ofisa Mwandamizi wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Philbert Ngoti, anasema udhalimu wa ujangili uliwakumba wanyamapori hao, hata kutikisa ustawi wao.

Takwimu za Shirika la Uhifadhi Duniani (IUCN), zinabainisha kuwa katika miaka ya 1970 Tanzania ilikadiriwa kuwa na faru 10,000 huku Hifadhi ya Taifa Serengeti pekee ikiwa na wanyama hao wapatao 700.

Sababu ni nini? Ngoti ambaye pia Mratibu wa Faru nchini, anawanyoshea kidole majangili kuwa ni sehemu ya mzizi wa tatizo lililobadili historia ya nchi na hata kuelekea kuwa hasi zaidi.

Anasema Tanzania ni nchi iliyotamba duniani kwa idadi kubwa ya faru, lakini kutokana na baa la ujangili, iligeuka kuwa na hifadhi ya kubahatisha ya wanyama hao, tukio la kiharamia lilizozikabili pia nchi nyingi duniani.

Kutokana na hali hiyo, Ngoti anasema serikali ilichukua hatua mbili kuu, ikiwa ni pamoja na ukali uliopitiliza katika ulinzi wa wanyamapori, ambao sasa askari wake wanaowajibika ni jeshi kamili.

Anasema serikali pia iliumiza kichwa kwa njia ya pili inayotokana na faru waliopelekwa ughaibuni Afrika Kusini wakawe mahali salama na rahisi kuzaliana, wakiwa katika hesabu ya wanandugu tisa waliorejeshwa katika hifadhi za nyumbani Novemba 10 mwaka juzi.

Ofisa huyo anabainisha kuwa kuchukuliwa kwa hatua hiyo ya nchi kupeana faru, ni sehemu ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Kusimamia Viumbe Vilivyo Hatarini Kutoweka (CITES).

Ngoti anasema kuwa katika maisha hayo mapya, faru hao waliotoka ughaibuni na ndugu zao wa nyumbani, jumla yao ilifika 190 kwa takwimu zilizoishia Machi mwaka jana, huku lengo kuu la nchi ni wafike 205 kufikia mwaka 2023, yaani miaka miwili ijayo.

Mtaalamu huyo wa wanyamapori, anafafanua mchakato wa kuzaliana kwamba mimba ya faru inachukua kati ya miezi 15 na 16. Kwa lugha rahisi, ni wastani wa mwaka mmoja na robo.

Anasema mikakati iliyochukua imesaidia kuongeza idadi ya wanyama hao nchini, akiweka wazi kuwa mwaka 2018, nchi ilikuwa na faru 161 na hadi kufikia Machi mwaka jana, walifikia 190, likiwa ni ongezeko la faru 29 ndani ya miaka miwili.

Ngoti anasema mpango uliopo ni kuwatawanya ndugu wa Faru Fausta katika makazi mapya ndani ya hifadhi za taifa: Burigi-Chato na Arusha.

Anabainisha faru sasa wanalindwa kwa kifaa maalum cha kufuatilia mienendo yao na taarifa zao kupokewa kwenye vituo mbalimbali kwa teknolojia ya kisasa.

Hakika, tunapoadhimisha miaka miwili ya kifo cha faru Fausta, tuna kila sababu ya kuipongeza serikali kupitia mamlaka zake za uhifadhi, kwa jitihada kubwa zilizofanyika kuwanusuru wanyamapori dhidi ya ujangili!

SAFU

## KONA YA UKWELI

# Tanzania inahitaji utitiri vyama vingi?



Na Thobias Mwanakatwe

NI mwaka wa 29 tangu Tanzania iliporejesha mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992. baada ya kufutwa kwa mujibu wa sheria mwaka 1965 kwa maelezo kuwa vyama vingi vilishindwa kufanya siasa.

Mwaka 1992, Katiba ilirekebishwa na kifungu cha 3 kifungu kidogo cha kwanza kinasomeka 'Jamhuri ya Muungano ni nchi ya kidemokrasia na yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa.'

Tanzania imeandikisha vyama vya siasa takribani 22 vyenye usajili wa kudumu baada ya kuukubali mfumo huu. mfumo wa vyama vingi ulikuwapo nchini hata kabla ya Tanganyika kupata uhuru kwenye katiba iliyorithiwa ya Westmister mwaka 1961.

Uwapo wa mfumo huu unasaidia kukibana chama tawala na serikali yake kutolala usingizi kwa kukosoa na kuibua madudu mbalimbali.

Lakini swali la kujiuliza ni je, misingi ya kuanzishwa kwa vyama vingi vya siasa inazingatiwa na vyama husika hasa kufanya shughuli za kisiasa kwa mujibu wa sheria badala ya kuwa 'vyama mfu' vya kulala usingizi na kila wakati kulia kupatiwa ruzuku ya serikali?

Itakumbukwa katika miaka ya hivi karibuni tumekuwa tukishudia kukiukwa kwa misingi ya kuanzishwa kwa vyama vya upinzani kutokana na baadhi ya vyama kutozingatia masharti ya usajili wake kama vile kuwa na ofisi, wanachama pamoja na kufanya uchaguzi wa viongozi wake kwa muda mwafaka.

Wapo baadhi ya wanasiasa na vyama vyao badala ya kusimama katika misingi ya kidemokrasia, lakini wao wamekuwa ndo wachochezi wakubwa wa vurugu katika vyama vyao. Wengi wao wamekaa muda mrefu katika uongozi, lakini vyama vyao vinaendelea kuwa dhaifu ikiwamo kuongozwa kwa misingi ya kifamilia na havina mvuto kwa wananchi kiasi cha kukosa kura kwenye uchaguzi.

Kwa muda mrefu tumeshuhudia vyama kadhaa vya upinzani vikishindwa kuibua hoja na kukosoa utendaji wa serikali na chama tawala katika uendeshaji wa nchi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo pale inapoonekana kuna madhaifu.

Ni ukweli kwamba sio lazima chama cha siasa kipinge kila jambo linalofanywa na serikali ya chama kilichopo madarakani, lakini vyama vyetu vingi vimekosa uthubutu wa kuifuatilia serikali na kuikosoa.

Huko nyuma vyama kadhaa vya siasa vilifutwa kutokana na kushindwa kutekeleza majukumu yake na sheria kwa ujumla ya vyama vya siasa. Baadhi ya vyama hivyo ni PONA, TPP, CHAUSTA na PPT Maendeleo.

Wakati umefika kwa vyama vya siasa viongozi wake wahakikishe wanatimiza wajibu wao wa kuwa wafuatiliaji na wakosoaji wa serikali katika utekelezaji wa sera, sheria na miradi ya maendeleo kwa lengo la kuhakikisha kwamba utekelezaji huo unaleta maendeleo kwa wananchi na taifa kwa ujumla.

Wiki iliyopia Waziri Mkuu mstaafu, Cleopa Msuya alizungumzia suala na utitiri wa vyama na kusema hakuleti afya katika nchi.

,Alisema inashangaza kuona Tanzania kuna utitiri wa vyama kati ya 19 hadi 22 vilivyosajiliwa katika ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini.

"Sasa unajiuliza Tanzania hii demokrasia tunaitafuta kwenye vyama 22 ni nini hasa,wakati bado tuna sehemu ambazo watu wana njaa, bado tuna sehemu ambazo wabunge wanaomba barabara zijengwe, hivi kweli 'seriously' unasema tuna haja ya vyama vingi? alihoji.

Alisema demokrasia anayoiona isiwe ya utititri wa vyama vingi vya siasa bali kutafutwe njia ya kuwa na vyama vichache kama vitatu au vinne na isiwe kulazimisha bali wananchi waulizwe kwa kupiga kura na mwisho wa matokeo ya kura utakuta kuna vyama ambavyo hawavitaki.

"Kuna vyama katika hivi 22 kwenye uchaguzi havikupata hata kura 1,000, nchi nyingine wanachokifanya vile ambavyo havikufikia kiwango fulani wanavifuta na kubakia vile ambavyo kiasi fulani vinakubalika," alisema.

Aliongeza kuwa kule ambako tumefungua milango kwenye utitiri wa vyama na utitiri wa wanasiasa imekuwa ni shida, inahitaji kuwa na vyama vichache kwani si wengi wanaoelewa dhana ya kuwa na vyama vingi na wanaweza kuwa serikali mbadala kwa kuchunguza makosa ambayo yanafanywa na serikali iliyopo.

Msuya anasema mataifa kama Ujerumani, Korea Kusini, Japan, Malaysia na Singapore yameweza kupiga hatua haraka kimaendeleo kutokana na ushirikishaji wa wananchi katika maendeleo lakini si kwa kuwa na utitiri wa vyama. Nakubaliana na na Msuya kwamba utitiri wa vyama hauna maana katika nchi,tubaki na vyama vichache tu visivyozidi vitano.

Sote tumekuwa tukishuhudia baadhi ya vyama vimekuwa vikiibuka tu inapofika wakati wa uchaguzi mkuu, huku vikishinikiza kupewa fedha kama ruzuku kutoka serikalini.

Kukaa kimya na kuibuka wakati wa uchaguzi huwa kunazua maswali mengi kwa wananchi kwamba vyama hivi kweli vinafahamu fika jukumu lao au vinaibuka wakati wa uchaguzi kutokana na viongozi wake kutafuta maslahi fulani?

Ifike wakati sasa vyama ambavyo havifanyi kazi yake ipasavyo viondolewe katika usajili na kama hilo gumu kutekelezwa, itungwe sheria ambayo itavifanya vyama vinavyokosa sifa vikafutwa. Kwa nini kwa mfano tusibaki na CCM, CHADEMA, ACT-Wazalendo, NCCR_Mageuzi na CUF?.

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2005@yahoo.com**

## DARASA LA NDOA

# MALEZI BORA NI KINGA DHIDI YA UKATILI WA KIJINSIA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

FAMILIA ni msingi wa maadili mema katika jamii na taifa. Maendeleo yanahitaji watu waadilifu.Uadilifu huo unajengwa kuanzia ngazi ya familia. Tunaishi katika jamii ambayo kuna migogoro na kuvunjika kwa ndoa nyingi.

Halikadhalika, ombwe la malezi ya watoto ni kubwa katika jamii yetu ya leo, kwani wazazi wengi hawana muda na watoto wao. Hali hii inaathiri sana makuzi ya watoto na kuchangia ongezeko la vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Ukatili ni tatizo la kimaadili, hivyo, vitendo vya ukatili wa kijinsia vinapoongezeka katika jamii ni kiashiria cha mmomonyoko mkubwa wa maadili.

Tabia na mienendo yetu inajengwa katika familia. Wanasaikolojia wanasema, zaidi 60% ya wewe na mimi tulivyo leo ni matokeo ya makuzi wakati wa utoto. Hivyo, watu wakatili wametengenezwa katika familia.Ni vema ieleweke wazi kuwa, jukumu la kujenga jamii na taifa letu ama kulibomoa, tunalo sisi wazazi, walezi na wanajamii.

Wakati umefika sasa jitihada za kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia zisiwe za kutoa matamko, kutengeneza mabango, fulana au vipeperushi tu na kutafuta umaarufu, bali jitihada hizi lazima ziende sambamba na dhana nzima ya malezi katika ngazi ya familia. Ustawi wa taifa unaanzia nyumbani kwa kuwa uhai wa taifa unategemea uhai wa familia.

**Malezi ya mtoto**

Mtoto ni malezi. Ni wajibu wa Baba na mama kuwapa watoto malezi bora. Malezi bora ni ufunguo na urithi wa maisha kwa mtoto. Taasisi, jamii na taifa bora la kesho, linategemea malezi bora yanayotolewa na taifa bora la leo. Malezi bora huanzia katika ngazi ya familia.Malezi bora ndiyo mwelekeo sahihi wa maisha ya mtoto, kwani kesho bora ya mtoto inajengwa na leo bora ya wazazi bora.

Familia ni msingi na kitengo kinachomtengeneza mtoto kiroho, kimwili na kitabia (attitudes). Vitengo vingine kama taasisi za dini au shule husaidia tu na kuendeleza msingi uliojengwa na wazazi. Kwa hiyo, kazi ya vitengo vingine inaweza kuwa nyepesi au ngumu kutegemea na jinsi kitengo cha msingi yaani familia kilivyotunza wajibu wake wa malezi.

Wazazi wanapaswa kuwa mfano bora wa matendo, kauli na mienendo yao. Watoto wa leo ni raia na viongozi wa kesho; ndio watakaokuwa sifa au aibu kwa wazazi wao, kwa familia yao, kwa jamaa na taifa lao.

Waswahili wanasema, "mtoto umleavyo ndivyo akuavyo". Ni wajibu wa wazazi kuwapa watoto wao malezi yatakayowaandaa kuishi maisha ya kumpendeza Mungu na binadamu wengine.Wazazi msikwepe wajibu wa kukemea pale inapobidi. Watoto wote wasioadabishwa na wenye tabia mbaya ni udhia, mzigo, karaha, na fedheha kwa wazazi na jamii. Ukimdekeza mwanao iko siku atakuaibisha na kukusababishia maumivu usiyoyatarajia.

Mtoto mwenye malezi mabaya atakuwa na maisha magumu hapo mbeleni. Watu wasiowajibika, magaidi, wakatili, wanyanyasaji, vibaka, walevi, kundi la watoto linalojiita, "watoto wa Ibilisi"kama ilivyoripotiwa na vyombo vya habari hivi karibuni, wahuni wa kila aina tulionao leo ni matunda ya malezi mabaya.

Wazazi wawe na muda na watoto

Wazazi msiridhike tu na kule kuwapatia watoto wenu mambo ya ulimwengu huu. Watoto wenu wanahitaji uwepo wenu wakionja hisia, mapigo ya mioyo yenu, hali ya kujali na kuthamini maendeleo ya kiroho, kimwili, kiimani, kisaikolojia na kadhalika. Upendo na muda unaopatikana kwa ajili ya watoto wenu ni zawadi kubwa isiyoweza kuthaminishwa na chochote. Mtoto hahitaji tu baba au mama bali anahitaji baba au mama anayejali na anayepatikana nyumbani. Baba na mama wasiwe kiwanda cha kuzalisha watoto na kuwatelekeza pasipo kuwajibika katika malezi.

Kuwa baba au mama ni jukumu kubwa. Kwa hiyo, ni muhimu sana wazazi wafahamu majukumu waliyonayo kwa watoto wao ili kujenga familia na jamii bora. Maadili mema ni uhai kwa familia, jamii na taifa. Hatuwezi kuendelea kiroho, kimwili, kiuchumi, kisiasa na kijamii pasipokuwa na maadili yanayompendeza Mungu na binadamu wenzetu. Hivyo, ili tuwe na taifa imara la watu waadilifu na wasio wakatili, lazima mkazo uwekwe katika malezi ngazi ya familia.

**Elimu dunia na elimu ya kiroho**

Watoto waliozaliwa kama raia wa dunia hii wanapaswa kutambua kuwa uraia wao halisi uko mbinguni. Hivyo, lazima watoto waandaliwe kwa ajili ya hatima hiyo pia. Jitihada za kuwapatia watoto wetu elimu dunia ni muhimu sana ziende sambamba na kuwapatia elimu ya kiroho (kuhusu Mungu) ili watoto hawa wawe baraka sasa na hapo baadaye. Malezi bora ni uwekezaji na urithi muhimu katika maisha ya mtoto.

Tutengeneze kizazi chenye kumpenda Mungu na binadamu mwingine. Vinginevyo tutakuwa na watu ambao ni mzigo usiobebeka kwa familia yenyewe, jamii na taifa kwa ujumla. Waswahili wanasema, "mkunje samaki angali mbichi". Ukiwa mzazi au mlezi unaalikwa uwashirikishe watoto imani yako kuhusu Mungu, upendo wako kwa jirani na tumaini la maisha mema ya baadaye.

**Uhuru wa kuamua**

Tuwape watoto wetu uhuru wa kuamua, kuchagua, kutoa mawazo kuhusu maisha yao, lakini watoto wapewe uhuru wenye mipaka. Uhuru usio na mipaka matokeo yake ni vurugu, fujo na uharibifu. Tuwasaidie watoto na vijana wetu wasiendekeze tamaa, starehe na anasa, kiu ya mali na utajiri pasipo uwajibikaji wa kutosha. Tuwasaidie kufahamu kuwa maisha mazuri yanatengenezwa kwa kuwa na nidhamu binafsi ya maisha, juhudi, subira na uvumilivu, na kumtanguliza Mungu katika kila jambo.

**Familia ni shule**

Familia ni kitovu cha malezi, shule ya Neno la Mungu, sala na kitalu cha maadili mema. Wazazi tunapaswa kuwa mfano mwema kwa watoto wetu, kwani watoto hujifunza zaidi kwa kuona na kusikia. Ikumbukwe kwamba, siku zote matunda mema hutoka katika mti bora. Watoto wenye malezi bora; walioelimishwa kumcha Mungu watakuwa na utii, upendo, na msaada mkubwa kwa wazazi wao katika umaskini na uzee wao na kufanyika baraka kwa watu wengine pia. Suala la malezi ni ajenda muhimu katika jitihada za kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia katika jamii.

**[Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066].**

# MAISHA

DESEMBA 5, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 13

**Mashati yaliyobamba mwaka 2021**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Fuata haya unapotaka kuwekeza katika nyumba



Ukurasa 12



## USO UNAONG'AA

# Chumvi inatosha kukupa furaha

Ukurasa 14

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA




### VITU TISA

GARI
MWANASESERE
KOFIA
MPIRA
JAHAZI
KISHADA
SOKSI
PENSELI
SURUALI


| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | T | A | N | G | A |
| ■ | I | ■ | ■ | A | ■ |
| I | M | O | ■ | W | ■ |
| ■ | I | ■ | H | A | I |
| ■ | Z | ■ | ■ | N | ■ |
| L | A | M | B | A | ■ |

## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
DOA, IPO, TIMBA, PANDE, PEPONI, DODOMA


## TOA TOFAUTI 5




## PAKA RANGI




## AMSHA AKILI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juma alikwenda alikwenda matembezini eneo la ufukwe wa bahari akiwa na baba yake. Walipofika ufukweni Juma aliwaona watu wengi wakiwa katika harakati nyingi, wengine waliogelea baharini, wengine walikaa ju ya mchanga mweupe na baadhi walikuwa wakitembea huku wakila vyakula vitamu. Juma alishangaa sana kuona hali ile, aliona watu wakila mihogo, Ice Cream, viazi na juisi za aina mbalimbali.

**Juma:** Baba mbona hakuna chakula kingine huku?

**Baba:** Vyakula hivi ndivyo vinapatikana huku kutokana na urahisi wake wa kuandaa

**Juma:** Kwani wali hawawezi kuupika huku ufukweni?

**Baba:** wanaweza lakini si mahali pake sahihi

**Juma:** Mbona mwalimu alituambia Mgaagaa na upwa hali wali mkavu?

**Baba:** Mwanangu huo ni msemo tu, unamaanisha kila anayehangaika hawezi kukosa kile anachokitafuta.

**SWALI**

Daraja la Umoja linapitikana Mkoa gani na mpaka wa nchi zipi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Walinyang'anywa nafasi zao, Mungu akawapa nzuri zaidi

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na gurudumu la Maisha Ndivyo Yalivyo. Leo nimalizie sehemu ya mwisho ya shuhuda za watu waliopoteza nafasi zao, chimbuko likianzia katika ulimwengu wa roho.***

Wiki iliyopita tuliona binti aliyeachwa na mchumba siku ya kufunga ndoa yake, lakini cha ajabu mchumba huyo huyo akajikuta akiwa ni mlinzi wake baada ya kuolewa na mtu mwingine. Sikia tena shuhuda hizi ili kujenga imani yako kuhusu nafasi au cheo ulicho nacho.

Kijana mmoja alikuwa akifanya kazi katika benki moja kwenye nafasi ya Mtunza Fedha. Ikatokea amefukuzwa kazi. Akamwendea baba yake wa kiroho kutaka ushauri. Akamwambia amekuwa akitoa sadaka ya fungu la kumi, kwanini afukuzwe kazi. Naye akamshauri aende kwenye nyumba ya ibada akamuulize Mungu, imekuwaje nafukuzwa kazi na fungu la kumi nakupa wewe?

Kijana akaanza kuomba kuanzia asubuhi hadi jioni. Mungu akishakupa nafasi hawezi kukunyang'anya. Alipomaliza maombi na wenzake, akachukua teksi kuelekea nyumbani. Kufika mbele teksi ikasimama na kumpakia mtu mwingine.

Wakati wanaendelea, yule jamaa aliyepandia njiani akamuomba simu yake aitumie kumpigia jamaa yake wa Marekani. Kijana akafoka; "mimi nimefukuzwa kazi, kwanza simu za nje zinakula vocha sana.

"Sitaki, nimebakiwa na muda mdogo wa maongezi kwenye simu". Jamaa akasisitiza kuwa anaomba tu simu apige kisha atamlipa baadaye. Jamaa alizidi kufoka, lakini akambembeleza, akakubali. Akampa simu na kumpigia huyo mtu wa Marekani.

Alipomrudishia simu, kuangalia salio akakuta hela yote imeisha. Akaanza kulalamika, "nilikuambia simu ya nje inakula hela sana, ona sasa". Jamaa hapo akawaza amefukuzwa kazi na hapo vocha imekata. Akafika mahali pa kushukia wakaachana pale.

Kufika nyumbani akakaa huku anawaza afanyeje. Ghafla simu ikaita, kuangalia namba ni ya Marekani. Akapokea akamwambia, yule uliyekuwa unaongea naye kwenye simu alishaondoka kwake, usinisumbue, jamani sitaki shida! Huyo wa Marekani akamwambia, nataka nikuambie kitu, tulia, una shida gani?

Kijana akamjibu, "mimi nimefukuzwa kazi". Jamaa wa Marekani akamwambia tunataka utusaidie kazi. Namba ya yule aliyenipigia nimeipoteza. Sisi ni shirika la fedha la Marekani. Tunataka tufungue tawi letu Afrika ili wewe uwe Mkurugenzi Kanda ya Afrika. Umesomea mambo ya fedha?

Akajibu, ndiyo, ni kweli. Kuanzia leo tumekupa kazi utasimamia bara la Afrika. Akashangilia na kwenda kutoa ushuhuda kwenye dhehebu alikokuwa anaabudu. Jamaa huyu alikuwa akiimba nyimbo tano kwa dakika moja, kisa furaha kwa muujiza aliopata. Hakika Mungu alikuwa amemtengenezea nafasi.

Msomaji wangu, wapo watu ambao hupata misukosuko mingi lakini hiyo inatokea ili Mungu awatengenezee nafasi. Baada ya kufukuzwa kazi, utapata kazi nyingine nzuri zaidi. Baada ya kuteseka kwenye ndoa, yapo maisha mazuri zaidi mbele yako!

Sikia ushuhuda mwingine. Kijana mmoja akaenda kwenye ibada dhehebu anakosali. Alipata viza kwa shida sasa akataka kiongozi wake wa kiroho amuombee aweze kwenda Marekani. Wakati anaomba, roho wa Mungu akamwambia baraka za kijana haziko Marekani bali ziko Mbulu.

Yule kijana ambaye alikuwa ameambatana na mama mzazi alipoambiwa akafoka, "ziko Mbulu?" Mama yake akamwambia, chochote alichokuambia mtumishi wa Mungu, wewe fanya. Yule kijana akakubali akaenda Mbulu.

Akasema, "nampa muda huyo mtumishi, ole wake unabii usitimie. Na viza yangu ni ya miezi sita, ikiisha muda wake, tutajuana. Akawa anaishi hotelini huko Mbulu.

Wakati anakula akashangaa mbele yake kuna ugomvi kati ya mwarabu na mwafrika, wanapigana. Sauti ikamuinua kusema, nenda kaamue ule ugomvi. Jamaa akawaachanisha. Baada ya hapo yule mwarabu akafurahi, akamwita, naye akajibu kwa hasira, niache kwanza. Kwanza wewe nikikuona nakufananisha na Osama Bin- Laden. Akamwambia mimi ni mtu mzuri.

Nimekuja hapa kwenu nataka nianzishe kampuni ya mafuta na mshahara wa kwanza kukupa ni dola za Marekani 10,000 kwa mwezi. Kijana akashangaa akidhani ni utani. Jamaa akaandika hundi dola 10,000. Baadaye zikapanda hadi dola 60,000. Nafasi yako ipo na chochote unachotaka kipo!

***Msomaji, bila shaka umefurahia shuhuda hizi kuhusu nafasi ambayo Mungu ameweka mbele yako kwa maisha yako. Je, una maoni,kisa? Tuma ujumbe mfupi 0715268581***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# TBS mko wapi bidhaa feki zinazagaa sokoni?

NI kawaida sasa unapoingia kwenye duka na kuulizia unachotaka kisha kuonyeshwa bidhaa za aina mbili, moja halisi na nyingine ni nakala ya kile halisi, yaani ubora wake uko chini.

Kinachoshuhudiwa ni muuzaji ananadi bidhaa zinazouzwa kwa bei ghali na zenye bei nafuu, ambazo ni feki.

Mbaya zaidi, hali hii iko hadi kwenye bidhaa za vyakula yakiwamo maziwa ya watoto. Haishii hapo, iko hadi kwenye bidhaa za vifaa vya umeme kama simu na vya kufunga kwenye nyumba.

Kwenye nguo na viatu nako ni hivyo hivyo kwamba kuna halisi na isiyo halisi huku uzoefu ukionyesha bidhaa zisizo halisi huuzwa kwa bei ya chini na kukimbiliwa na wengi pasi na kujua kwamba havidumu na husababisha madhara kwa watumiaji.

Mbaya zaidi wakati mwingine wafanyabiashara wanauza ambavyo siyo halisi kwa kwa bei ya bidhaa halisi, wakitumia mwanya wa wananchi kutokuwa na uelewa wa kutambua bidhaa halisi na bandia.

Kinachoshuhudiwa sasa mitaani na kwenye maduka ni kutapakaa kwa bidhaa bandia kunanozua maswali mengi "mamlaka zinaona hili na kama zinaliona zinachukua hatua gani?"

Inakwenda mbali zaidi ya hapo kwamba kwa nini bidhaa ambazo hazina viwango au viwango hafifu zinaruhusiwa kuingia nchini? Katika hizo ni ngapi ziko salama kwa watumiaji? Ni ngapi zinasababisha madhara ya kiafya au kuteketeza nyumba au hata madhara mengine ya kimazingira?

Ni sahihi kusema huenda nchi ingeuzwa dampo la bidhaa zisizo na viwango vya kutosha? Ni kwa nini wananchi waingie gharama kwa kununua bidhaa hizo ambazo watatumia muda mfupi kisha zinaharibika?

Unapoenda Kariakoo unakutana na bidhaa za aina hii kwa kiwango kikubwa na mbaya zaidi watu wanaibiwa kwa kuambiwa ni halisi huku wanaonufaika wakiwa ni wafanyabiashara wachache na nchi zinakotoka.

Hili linanikumbusha majukumu ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ambayo ni kukuza viwango katika sekta ya viwanda na biashara kwa bidhaa zote zilizoagizwa na zilizoko viwandani katika kuingia soko la Tanzania.

Pia kuna mpango wa ukaguzi wa awali kwa usafirishaji wa bidhaa unaotumika kuratibu bidhaa zinazosafitishwa katika nchi husika ili kuhakikisha bidhaa zote zinazoingizwa nchini zinaendana na taratibu za kiufundi zilizokubaliwa Tanzania na nje kabla ya usafirishaji.

Lengo la msingi la kutumia mpango wa viwango ni kuhakikisha kuwa bidhaa zote zinazoingia Tanzania zinakidhi usalama wa afya, kulinda mazingira kwa mujibu wa taratibu za kitaalamu, kukidhi matakwa ya mpango wa uhakiki awali wa usafirishaji unahitaji msafirishaji apate hati ya viwango iliyotolewa na TBS kabla bidhaa husika haijaondoka nchini.

Mambo muhimu yanayotakiwa kufanywa ni ukaguzi wa bidhaa kabla ya usafirishaji, kupima sampuli na uchambuzi katika maabara zinazokubalika, ukaguzi wa taratibu za uzalishaji, mapitio ya kulingana na kanuni, utoaji wa hati ya kuzingatia ubora au ripoti zisizo na ubora unaofaa.

Majukumu ya waagizaji/wauzaji ni kuhakikisha wauzaji wanaelewa mahitaji ya uagizaji bora na kwamba mizigo yao inaambatana na upatikanaji wa cheti cha ubora.

Pia kuhakikisha bidhaa zinakidhi kanuni na mahitaji ya ubora wa bidhaa Tanzania kabla ya usafirishaji kwa kupata cheti kinachohitajika kuthibitisha ubora kutoka kwa mtoa huduma na kukosa kufanya hivyo atapewa adhabu na gharama za ukaguzi kufanyika nchini na kama haijafikia viwango bidhaa itarudishwa nchi ilikotoka kwa gharama za mwagizaji.

Kwenye maandishi mambo mazuri yapo, lakini shida iko kwenye utekelezaji ambako kunazua maswali mengi kwamba tunakwama wapi? Licha ya kazi nzuri inayofanywa na TBS bado hali iko ilivyo.

Kuna haja TBS, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) na nyingine kuona hili ni tatizo kubwa na kuchukua hatua.

Hata bila kufika Kariakoo, vipo viwanda vinazalisha bidhaa za aina hii na zinaingia sokoni, zikipita kwenye mipaka ikiwamo bandarini na kuingia sokoni.

Ni muhimu hatua zikachukuliwa kuepusha nchi kugeuka kuwa dampo la bidhaa feki ambazo zimejaa kwenye maduka mengi kwa sasa.

Bila kuchukua hatua, wananchi watazidi kuumia huku afya zao zikiwa hatarini pia kutokana na matumizi ya bidhaa bandia.









ILIKUWA siku ya furaha kwa Amosi Kuboja na Prisca Bita baada ya kufunga ndoa hivi karibuni katika Kanisa Katoliki Kibada jijini Dar es Salaam na kufuatiwa na tafrija iliyofanyika katika ukumbi wa Kobe ndani ya uwanja wa Sabasaba. **PICHA: MIRAJI MSALA**







# MITINDO

Na Christina Mwakangale



# Mashati yaliyobamba 2021

MWAKA 2021 umefika ukingoni ukiwa unaacha alama nyingi za mafanikio katika tasnia ya mitindo.

Ndani ya mwaka huu, tumeshuhudia mitindo mingi ya nguo yikishika kasi na kufanya dunia watu waone dunia ni sehemu nzuri ya kuishi na kuonyesha furaha.

Hata hivyo, hakuna atakayesahau kwamba mwaka 2021 ulitoa mtindo mipya ya mashati na jinsi ya uvaaji wake na kumfanya mtu kuonekana mtanashati zaidi.

Wabunifu walifanya kazi kubwa kubuni aina ya nguo hizo zitakazowavutia wateja pamoja na kuuweka uwanja mpana wa kuchagua wapi waende, nini wafanye na usafiri gani watumie pindi wanapovaa nguo hizo.


Kwa ujumla mashati ya mistari na rangi nyepesi ndio yalibamba mwaka 2021, watu wengi wameonekana wakifurahia maisha wakiwa na nguo hizo za kuvutia.

Tunaweza kusema mwaka umeanza na kumalizika ukiwa ni mwendo wa mashati pekee na dunia ilisimama kwa vazi hilo.




## UREMBO

**Na Mary Geofrey**



# USO UNAONG'AA

## Chumvi inatosha kukupa furaha





SURA yenye ngozi laini na mwonekano wa kuvutia ni vitu ambavyo wanawake wengi wanaojijali wanapenda kuwa navyo.

Kutokana na hitaji hilo kuwa kubwa, baadhi ya wanawake wanatumia vipodozi vyenye kemikali hatari kwa ajili ya kuweka sura zao katika hali ya kuvutia zaidi.

Hata hivyo, watalaam wa kiafya wanaonya matumizi ya vipodozi vyenye kemikali kwa ajili ya urembo, badala yake wanapendekeza kutumia njia za asili ambazo ni salama kwa afya.

Leo tunakuletea namna ya kufanya 'scrab' (kuchua) uso kwa kutumia chumvi na maji ya baridi.

Utumiaji wa chumvi ni wa salama zaidi na watumiaji wamethibitisha hilo kwa asilimia 99.

Matumizi ya chumvi kama `scrab' yanakupa matokeo mazuri ikiwapo kuiweka ngozi yako kuwa ya kuvutia na nyororo. Matumizi yake yanakupa faida kwa kuondoa chunusi, ukavu katika ngozi, mafuta usoni na hata kuondoa ngozi iliyokufa usoni.

**Mahitaji**

Chukua chumvi ya unga kijiko kimoja cha chakula, changanya kwenye maji kiasi na kisha safisha uso kwa mtindo wa kusugua.

Tumia kitambaa laini ambacho kimeloanishwa na maji, kisha chovya kwenye chumvi na sugua kwenye uso taratibu pia unaweza kutumia hata mwilini.

Baada ya kujipaka katika uso weka pembeni kitambaa kisha anza kujisugua kwa kutumia viganja vya mikono yako, fanya hivyo hadi utakapoona taka zinatoka, halafu kaa kama dakika tano na uoshe uso kwa maji safi.

## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# PERA NI TIBA

## ndani yake kuna maajabu mengi ya kiafya

MAPERA ni moja ya matunda yanayopatikana kwa wingi nchini, lakini huwa hayapendelewi kwa sababu ya tunda zake kuwa ngumu wakati wa kutafuna.

Hata hivyo matunda haya yana faida kubwa kwa afya ya mwili wa mwanadamu.

Mapera unaweza kuyala yenyewe au kuyasaga na kuwa juisi na unapotumia mwili unapata faida lukuki.

**Faida zake**

Mapera yana utajiri mkubwa wa Vitamin C ambayo ni muhimu sana katika mwili wa mwanadamu.

Ni kinga nzuri ya kisukari kwa sababu ulaji wa watu wengi unawaweka katika hatari ya kupatwa na ugonjwa huo.

Matumizi ya mapera yanapunguza hatari ya kupata ugonjwa wa kisukari kwa sababu yana Fibre inayopunguza sukari kwenye damu.



Mapera yana utajiri mkubwa sana wa Vitamin A au Retinol ambayo ni muhimu sana katika kusaidia kuona vizuri. Hivyo basi kama ilivyo kwa karoti, mapera yanasaidia sana katika kuongeza na kuimarisha uwezo wa mtu kuona.

Yana madini yaitwayo Folate ambayo husaidia katika kurutubisha mayai ya uzazi na hurekebisha kiwango cha shinikizo la damu.

Madini ya potassium, yaliyomo ndani ya mapera yanasaidia katika kuweka sawa na kuzuia shinikizo la damu.

Mapera yana madini ya shaba ambayo ni mazuri katika kusaidia ufanyaji kazi wa tezi ziitwazo thyroid.

Mapera pia yana utajiri mkubwa wa madini ya manganese ambayo yanausaidia mwili katika kunyonya ama kupata virutubisho muhimu kutoka kwenye vyakula tunavyokula.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Fuata haya unapotaka kuweweza katika nyumba

## Namna ya kupangilia funguo za milango



NYUMBA za kisasa zinakuwa na milango yenye vitasa imara ili kuzuia mtu kuingia ndani kwa urahisi.

Hata hivyo kunatakiwa umakini wa kuweka funguo za milango ili kutosababisha kujichanganya na kushindwa kufungua milango pale inapotokea dharura ya haraka. Kutokana na umuhimu wake hizi ni baadhi tu ya mbinu za kupangilia funguo kwa ajili ya usalama.

**1:** Weka alama kwa kila funguo ya chumba ili iwe rahisi kuutambua. Unaweza kutumia plastiki ngumu ambayo unaweza kuandika majina ya vitu au watoto kama kitambulisho chako.

**2:** Weka funguo za akiba sehemu moja chumbani kwako kwa sababu ukiweka tofauti unaweza kuchanganyikiwa pale inapotokea tatizo.

**3:** Hakikisha funguo hazibaki kwenye kitasa nyakati za usiku ili kukurahisishia kufungua mlango haraka inapotokea tatizo.

**4:** Weka funguo sehemu inayotambulika haraka pale mlango unapufungwa ili uweze kuikumbuka haraka pale unapoona kuna tatizo limetokea.

UWEKEZAJI ni mchakato mzima wa kuiweka mali katika mfumo maalum wa kifedha kwa ajili ya tija zaidi ya baadaye inayoweza kuongezeka au namna fulani yenye kuleta faida baada ya muda fulani.

Ujenzi wa nyumba ni miongoni mwa maeneo muhimu yanayotumiwa na wengi kuwekeza.

Leonald Michal ni mshauri wa masuala ya uwekezaji, anabainisha kanuni bora za kuwekeza kwa tija.

Anashauri kwamba unapowekeza kwenye ujenzi wa nyumba, miongoni mwa mambo ya kuzingatia ni pamoja na kufahamu unataka kujenga nini kulingana na mahitaji katika uhalisia wa sasa na wa baadaye.

"Kutazama ni aina gani ya watu watakaotumia nyumba yako, shughuli gani ambazo zitakuwa zinafanyika katika nyumba husika ni muhimu. Kwa hiyo ni muhimu pia kushirikiana na mtaalamu aliyebobea katika usanifu.

"Pia kujenga kwa kuzidi uwezo wako huleta hasara ya kushindwa kumaliza ujenzi, sehemu nyingine kutotumika na kutokuwa na faida ya kutosha, kutumia pesa nyingi kwa kitu kisicho na faida na kuwa na gharama kubwa za uendeshaji wa jengo.

"Kujenga kwa kutokidhi mahitaji, huleta hasara kwa kulazimika kufanya upanuzi wenye gharama kubwa zaidi, kuacha nyumba na kutafuta nyingine, kutoridhika na kutokuwa huru zaidi. Ni muhimu kuhakikisha kwamba unachojenga kitaleta faida kwa kipindi hicho cha uwekezaji," anasema.

Anashauri kwamba ni vyema kujiuliza maswali kama je, kodi ambayo wapangaji wanailipa inaleta faida, mtaji uliotumika kujengea utakuja kujilipa baada ya muda gani, faida ya






kipesa itaanza kupatikana baada ya muda gani na je, nyumba yako itadumu kwa miaka mingapi?

Jambo lingine muhimu anasema unapowekeza katika sekta hiyo ya nyumba ni muhimu kufuata sheria na taratibu zote husika ili uwekezaji wako usibughudhiwe na mambo mbalimbali ambayo yanaweza kuhatarisha mchakato wa kupata faida kwa kujenga katika eneo linaloruhusiwa kisheria na kwa kufuata sheria na taratibu zote.

Pia anashauri kwamba makadirio ya gharama za ujenzi yatakusaidia namna ya kujipanga juu ya mtaji wa kukuwezesha kusonga mbele na kazi yako na kwamba si vyema kujenga kwa kubahatisha.

Ni muhimu kuiona faida katika mipango yako ambayo umeifanya kabla ya kuanza ujenzi.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
HIKI NDIO KIPIMO SAHIHI CHA UONGOZI 'KWELI!?'
KERO
USHAHIDI UPI UNAOKUSUKUMA KUNIONA MIMI 'MLA'RUSHWA!'
'HIKI NINI?
HALI YA HEWA IMEPOA HAKUNA JOTO, HAYA ZUA SABABU MPYA YAKUNIKERA!
'NNA NGIRI'
AFADHALI JOTO LINGEENDELEA ILI TUZIDI KUSHIKA ADABU ZETU!
INFWAKTI UMEFUNGUKA 'TRUU! ETI KIJIMVUA AKIJACHANGANYA KILA JIRANI ANAZIBUA CHOO MTAA HAUKALIKI
USWAHILINI NDIO ZAO WAKIONA MANYUNYU KAMA WAMEONA GARI YA MAJI TAKA! NAKEREKA KINOMA NIMEAMUA KUHAMA KUHOFIA KUMSINDIKA MTU MAKONDE
HAYO MATENDO YANAFANYIKA BILA KUHOFIA KUWA KUNA KORONA, TUNAMUALIKA KIPINDUPINDU AJE WASAIDIANE
KONDA SHUSHA NAONA KELELE TU WENGI WETU TUNA-MABANDA YA URITHI USWAZI HATA BAISKELI HAIPITI!
MNACHONGA TU WENYEWE FIUZI ZA PUA ZISHAFELI HATUSIKII HARUFU TUNAZIBUA TYUUU!
WE UNAOSEMA UME-HAMA HUNA LOLOTE UNAVIMBA HUMU ILI USIFIWE AU VIPI?
HII NDOTO SIJUI NILALE STAILI GANI IJE TENA! ETI NNA HELA NIME-ZUNGUKWA NA VIBINTI VINANIDANGIA
...IVI WE MSTAAFU UNADROO KUTWA MARA TATU KAMA DOZI HELA UNAZIPELEKA BAR GANI! 'ONA SURA ILIVYOKUKOMAA!'
LOH!
BENKI
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...BABA MKWE HALAZWI SEBULENI

## Wabunge wanawake Afrika wapitia unyanyasaji

**NEW YORK,** MAREKANI

ASILIMIA 40 ya wabunge barani Afrika wameshuhudia unyanyasaji wa kingono wakiwa kazini, na asilimia 23 wameshambuliwa kulingana na ripoti iliyoandaliwa na mashirika mawili ya kimataifa.

Ripoti hiyo ilisema mabunge mengi hayana mipango ya kuwawezesha wanawake kuzungumza kwa usalama, na kwamba unyanyasaji mwingi wa kingono na ghasia dhidi yao zilizofichuliwa zilidaiwa kufanyika katika majengo ya bunge.

Ilieleza wabunge wanaume ndio washukiwa wakuu dhidi ya wabunge wanawake, hasa wale kutoka vyama pinzani.

Wabunge wanawake walio na ulemavu , pamoja na wale walio chini ya umri wa miaka 40 , ambao hawajaolewa au kutoka makundi ya walio wachache wamedaiwa kukabiliwa na ghasia za viwango vya juu.

Idadi hiyo ilikuwa sawa na wafanyakazi wa viwango vya chini , ilisema ripoti iliyoandaliwa na Inter parliamentary Union (IPU) na American Parliamentary Union (APU), huku asilimia 18 wakisema walipokea maombi ya unyanyasaji wa kingono kutoka kwa wabunge wenzao. Ripoti hiyo inatokana na utafiti uliofanywa kwa wanawake 224 wanaofanya kazi katika mataifa 50 .Sera mpya za kukabiliana na unyanyasaji huo zimekuwa zikishinikizwa na mashirika hayo mawili.

**BBC**

# Wanachofanya Uganda baada ya kufanikiwa kuingia ndani ya DRC

**GOMA,** DRC

Vikosi vya Uganda kwa mara nyingine vimevuka mpaka wa magharibi mwa nchi hiyo na kuelekea Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Uvamizi wa hapo awali uligubikwa na utata mkubwa huku wanajeshi hao wakipambana na wanajeshi kutoka Rwanda,na kusababisha kuzorota kwa uhusiano wa nchi hizo mbili.

Kabla ya uvamizi huo, Rais Yoweri Museveni, akizungumza siku chache baada ya shambulio la kujitoa mhanga mwezi uliopita katikati mwa mji mkuu wa Kampala, alitoa wito kwa waliohusika kujisalimisha na kuahidi hata kama watu hao wametoka nje watakufa.

Serikali ililaumu kundi la waasi la Kiislamu linaloitwa Allied Democratic Forces (ADF), ambalo lilianzishwa nchini Uganda, kisha kulazimishwa kuingia DRC na inasema sasa ni sehemu ya kundi la Islamic state.

Jumanne ya wiki hii, jeshi la Uganda lilithibitisha kuwa lilifanya mashambulizi ya anga katika maeneo ya ADF, na kufuatia mamia ya wanajeshi wa Uganda walionekana wakivuka mpaka kuelekea DRC siku ya pili yake.

Serikali ya Congo ilisema kuwa imealika wanajeshi wa majirani zake nchini humo kwani ADF ni mojawapo ya makundi mengi yenye silaha yanayofanya uharibifu mashariki mwa DRC.

Kundi la ADF, lililofurushwa kutoka Uganda mwanzoni mwa miaka ya 2000, limekuwa likishambulia na kupora vijiji vya Congo, na kuua watu na kuwasajili watoto kwa nguvu kwa takribani muongo mmoja uliopita.

Mkazi wa mji wa Beni, karibu na mpaka, aliiambia BBC kwamba aliweza kusikia sauti ya milipuko.

"Kuna mapigano makali, wanajeshi wa Uganda waliingia kwa miguu na magari. Tumeona ndege zisizo na rubani zikiruka pia." Alisema mkazi huyo

Kanda za video zimesambaa kwenye mitandao ya kijamii zikionesha wanakijiji walio karibu na Beni wakitazama safu za wanajeshi wa Uganda wakipita.

Lakini maafisa kutoka serikali ya Uganda na Congo hawajatoa maelezo mengi, isipokuwa kuthibitisha uwepo wa wanajeshi wa Uganda.

Jeshi la Uganda limetoa msururu wa picha zinazoonesha safu za wanajeshi nchini DR Congo wakiwa wameandamana na magari ya kivita na vifaru.

Inasema maelfu ya wapiganaji wa ADF waliuawa katika mashambulizi hayo ya anga lakini haijatoa ushahidi wowote na haijawezekana kuthibitisha.Msemaji wa jeshi la Congo, Jenerali Leon Kasonga, alisema mapigano hayo yanatokea katika maeneo ya mbali, ikiwa ni pamoja na katikati ya msitu na Hifadhi ya Taifa ya Virunga, ambayo inaenea kwenye mpaka wa nchi hizo mbili.

Mwaka 1999 na 2000, wanajeshi wa Uganda na Rwanda, kila moja likiunga mkono kundi tofauti la waasi wa RCD, walipambana katika mji wa Kisangani nchini Congo.

Katika kile kinachojulikana kama vita vya siku sita, zaidi ya watu 1,000 wanasemekana kuuawa mnamo Juni 2000, wakati majeshi ya Uganda na Rwanda yakipigana kuudhibiti mji huo.

**BBC**



Wanajeshi wa Uganda wakivuka mpaka kuingia DR-Congo katika operesheni ya kukabiliana na wanamgambo wa ADF **(PICHA: BBC)**

# Guterres ataka uhuru uheshimiwe Sudan

**NEW YORK,** MAREKANI

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres, amehimiza mamlaka nchini Sudan kuheshimu uhuru wa kujieleza wa vyombo vya habari huku akiitaja nchi hiyo kuwa na chuki kwa wanahabari.

Hayo ni kwa mujibu wa barua iliyowasilishwa jana kwenye baraza la usalama, na kunukuliwa na shirika la habari la Ufaransa (AFP).

Limemnukuu Gutteress, akisisitiza wito wake wa kuachiwa huru kwa haraka na bila masharti kwa wale wote waliokamatwa na kuzuiwa kiholela na kukomesha kukamatwa kwa viongozi wa upinzani wa kisiasa pamoja na wanaharakati nchini humo. Mamia ya wanaharakati wa kisiasa, waandishi wa habari, waandamanaji na watu waliokuwa wakitazama maandamano ya kupinga mapinduzi ya Oktoba 25, walikamatwa. Katika mapinduzi hayo, Mkuu wa Jeshi Jenerali Abdel Fattah al-Burhan, alichukua madaraka kimabavu na kumuweka kizuizini Waziri Mkuu Abdallah Hamdok.

Kiongozi huyo alirudishwa madarakani baada ya lawama kutoka nchi mbalimbali pamoja na maandamano ya umma yanayoendelea kufanyika kila siku.

**BBC**

## SAFU/MAKALA

# Madhila ya mtoto anayebakwa na mwenye sauti ya baba yake

Na Elizabeth Zaya

KUNA mtu huwa anakuja chumbani kwangu usiku na ku... (anatamka madhila ya kufanyiwa ukatili), ananiziba usoni na ananibana mdomo, ananizuia kupiga kelele," msichana mwenye umri wa miaka saba anasimulia ukatili anaofanyiwa nyumbani kwao eneo la Igovu mjini Mpwapwa mkoani Dodoma.

Akiwa katika sauti ya chini, mwenye hofu na kuna baadhi ya hatua analia, mtoto huyo anasema mtu huyo amekuwa akiingia kwenye chumba chake cha kulala akiwa amejificha sura lakini sauti yake inafanana na ya baba yake mzazi.

Mtoto huyo anaendelea kusimulia, akitamka: "Wakati ananifanyia hayo (ukatili), ninaumia sana na hata siwezi kupiga kelele kwa sababu ananibana kwa nguvu na kunikandamiza kitandani.

"Nikiamka asubuhi ninachechemea, ninashindwa na kwenda shuleni. Nilimwambia mama yangu akanipeleka hospitalini, wakanichoma sindano kwenye kidole.

Mtoto huyo anasema amekuwa akiogopa kumweleza baba yake kuhusiana na mtu huyo anayembaka kwa kuwa sauti yake inafanana na baba yake.

"Sijamwambia baba kwa sababu ninaogopa atanipiga, nilimwambia mama ili amuulize ila sijui kama alimuuliza," anasema na kubainisha kuwa hatua iliyochukuliwa na mama yake ni kuanza kumfungia kwa kufuli usiku anapolala.

"Nikiingia kulala chumbani kwangu, mama alianza kufunga kufuli kwa nje na ananiwekea ndoo najisaidia ndani. Lakini yule mtu aliingia tena chumbani na kunibaka, sijui alitoa wapi funguo, na sauti ni ile ya baba yangu na alinitishia kwamba nikisema kwa mama ataniua.

"Baada ya mama kuona vile akaniuliza kama bado yule mtu ananifanyia tabia mbaya, nikamwambia ndiyo. Akanihamishia kwa jirani ndio nikaanza kulala na yule mtu hajaja tena kunifanyia hiyo tabia mbaya na kwa sasa bado nameza vidonge.

"Juzi bibi (jirani anakolala) alikuwa anatuogesha mimi na wenzangu, aliponigusa huku chini nilishtuka kulikuwa kunauma sana, akaniuliza kwa nini nashtuka, nikamwambia ukweli, akasema atazungumza na mama yangu," anasimulia.

Mama yake mtoto huyo anakiri kuwa na taarifa za madhila yanayofanyika dhidi ya mwanawe, lakini haamini kama baba yake anaweza kufanya kitendo hicho.

"Ni kweli mtoto aliniambia kwamba anabakwa na mtu ambaye anahisi ni mume wangu, kwamba ndiye huwa anasikia sauti yake akimtishia asipige kelele na asiniambie," anasema.

Hata hivyo, mama huyo anaamini kuwa kinachotokea dhidi ya mwanawe huyo huenda ni nguvu za giza kwa kuwa hata ujauzito wake ulitokana na kutumia dawa za kienyeji.

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Mpwapwa, Fadhili Molel, anakiri kuwa na taarifa za tukio hilo na alikuwa miongoni mwa waliokwenda kuzungumza na mtoto huyo mara tu baada ya kupata taarifa hizo.

"Na mimi nilikuja kuambiwa kwamba kuna mtoto anabakwa na baba yake mzazi, na kwa sababu mimi ninawajibika na kazi hizo, niliienda kumhoji, mtoto alieleza hivyo kama alivyokueleza wewe, kwamba amekuwa akibakwa usiku na amekuwa akisikia sauti ya baba yake," anasema.

"Mwalimu wake aliniambia kwamba hata mahudhurio yake yamekuwa siyo mazuri na siyo kawaida yake, na pale nyumbani kwao amehamishwa, analala kwa jirani.

"Bado ninaendelea kufuatilia na tukipata taarifa kamili, tutalifikisha suala hili mbele kwenye sheria, lakini tunashukuru kwa hatua za awali za wasamaria wema kumwondoa mtoto katika mazingira ya hatari," anasema.

Kwa mujibu wa Jeshi la Polisi nchini, matukio ya ubakaji na ulawiti wa watoto nchini kwa mwaka 2017 yalikuwa 759, mwaka 2018 yalikuwa 2,365 na mwaka 2019 yalikuwa 4,397.

Kwa mtazamo wa hesabu, takwimu za madhila hayo dhidi ya watoto zinaonyesha kuwa matukio yamekuwa yakiongezeka kila mwaka.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaidi Ali Khamis, anabainisha kuwa kati ya Januari na Septemba mwaka huu, watoto 6,168 walifanyiwa ukatili wa kijinsi na kati yao, 3,524 (takribani nusu) walibakwa.

Haki za watoto zinalindwa kimataifa kupitia mikataba mikubwa miwili ambayo ni Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (CRC) wa Mwaka 1989 na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC) wa Mwaka 1990, yote ikiwa imeridhiwa na Tanzania.

Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 inaelekeza wajibu wa serikali, wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vyote vya ukatili na ubaguzi.

**"Nikiingia kulala chumbani kwangu, mama alianza kufunga kufuli kwa nje na ananiwekea ndoo najisaidia ndani. Lakini yule mtu aliingia tena chumbani na kunibaka, sijui alitoa wapi funguo, na sauti ni ile ya baba yangu na alinitishia kwamba nikisema kwa mama ataniua.**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Mambosasa, Mahadhi, Fungo hadi Mwameja



Na Adam Fungamwango

**John Semainda, Hassan Mlapakolo, Mbaraka Salum, Athumani Mambosasa na Omari Mahadhi, hawa wote ni wa Simba. Niliowataja wote hapa wa Simba na Yanga ni moja kati ya vizazi bora vya makipa kuwahi kutokea kwenye historia ya klabu hizo.**

TUNAOPENDA soka bado tunakwenda uwanjani kuangalia kabumbu, na hata kuangalia kwenye televisheni kwa sababu dunia ya sasa ni ya teknolojia.

Zamani utaamua moja -- kwenda uwanjani au kusikiliza kwenye redio ya mbao 277. Ukisikiliza kwenye redio humwoni mchezaji. Utachoambulia ni kumsikiliza mtangazaji anavyomwelezea na kumsifia.

Ndiyo maana si wengi waliowaona wachezaji wa zamani ambao walikuwa na uwezo mkubwa kuliko hawa wa sasa.

Kwa sasa ukitazama baadhi ya mechi za Ligi Kuu, ni zile ambazo zamani zilikuwa kwenye ngazi ya daraja la tatu au la nne. Mchezaji hata kutuliza mpira hawezi, kupiga shuti tatizo na akipiga hakuna mpangilio wowote.

Kona zinapigwa hadi 15, kosakosa golini hakuna, achilia mbali bao. Timu inapata faulo kila baada ya dakika tano karibu na lango lakini hadi kipenga cha mwisho cha mwamuzi, hakuna bao la faulo.

Makipa wa sasa ni wazuri lakini wanadaka zaidi kwa kuvizia. Ni vigumu zaidi kuokoa hatari zaidi ya kufungwa. Unakuta kipa anasimama tu, mpira unatikisa nyavu.

Hii ina maana kuwa makipa wa zamani wanawashinda makipa wa sasa kwa kujituma, yaani kuruka kutoka upande mmoja kwenda mwingine. Walikuwa wanaruka kama nyani!

Walikuwa na uwezo wa kuruka kutoka upande mmoja kwenda mwingine, miguu ikiwa hewani, yaani anabadili uelekeo juu kwa juu, pia uwezo wa kuruka kwenda juu akiwa amenyooka, amepinda ameruka hewani, huku akiwa amejikunja kama samaki aina ya mkizi.

Hizi ndiyo staili za makipa wa zamani na huwezi kuzipata kwa makipa wa kisasa.

Zamani sifa namba moja ya kipa ilikuwa ni lazima ujue kuruka au kuchumpa kulia, kushoto, juu, na kunyumbulika. Halafu siri nyingine ni kwamba baadhi ya makipa wengi wa zamani walikuwa wana uwezo mkubwa wa kucheza sarakasi au walicheza mchezo huo wakiwa wadogo, na hii iliwasaidia sana kwenye kazi hiyo hasa kwenye eneo la 'diving'.

Pia inasemekana baadhi yao walikuwa wanacheza mchezo wa sanaa za mapigano kama vile 'karate', 'judo' na 'kung fu'. Hiyo iliwasaidia si tu kutawala golini, bali pia kuwa na uwezo wa kunyumbulika, kuruka na hata kuuwahi mpira kwa kupiga sarakasi. Hii iliwasaidia makipa wa zamani kuokoa mashuti yanayopigwa pembeni na kwa ghafla kwa sababu walikuwa na uwezo wa kuchumpa.

Leo tutawaangalia makipa wa zamani kuanzia miaka ya 1970 hadi mwishoni mwa miaka ya 1990.

Tunaanza na Elias Michael, Kitwana Manara, Muhidini Fadhili, Patrick Nyaga, hawa wote walikuwa wa Yanga.

John Semainda, Hassan Mlapakolo, Mbaraka Salum, Athumani Mambosasa na Omari Mahadhi, hawa wote ni wa Simba. Niliowataja wote hapa wa Simba na Yanga ni moja kati ya vizazi bora vya makipa kuwahi kutokea kwenye historia ya klabu hizo.

Wengine ni Bernard Madale na Dunia Adunisi wa Yanga, Idd Msakaa au Ally Yusuph na Juma Pondamali wa Pan African.

Zanzibar kulikuwa na makipa mahiri mwanzoni hadi mwishoni mwa miaka ya 1980, ambao ni Ramadhani Korosheni wa KMKM, Ally Bushiri na Ridhaa Hamis, wote wa Malindi.

Mwingine ni Kichochi Lemba wa RTC Kagera aliyekuwa ana staili ya kusimama golini akiwa amevaa kofia aina ya kapelo, kipa ambaye pia alikuwa na mbwembwe nyingi.

Makipa wengine ni Idd Pazi, Mohamed Mwameja, Steven Nemes, Offen Martin, Patrick Mwangata, Moses Mkandawire na Joseph Katuba ambao wote hawa wamehewahi kudakia klabu ya Simba.

Joseph Fungo, Bernard Madale, Hamisi Kinye, Rifat Said, Mfaume Athumani, Peter Manyika, Sadick Kalolola, Chachala Muya, hawa ni wa Yanga.

Pamba walikuwa na makipa mahiri ambao ni Madata Lubigisa, Paul Rwechungura na Juma Mhina, halafu Sigara ikawa ni kipa mmoja mahiri Mahmood Nyalusi.

Makipa Mkapa Maulidi na mwenzake Daniel Poka hawa walikuwa makipa mahiri wa klabu ya CDA ya Dodoma, Duncan Mwamba aliidakia African Sports, Salim Waziri, Said Jack, Hamisi Makene wa Coastal Union.

Nyota Nyekundu walikuwa na makipa wao maarufu, Morris Nyuchi na John Bosco, Ishaka Majaliwa alikuwa kipa wa Majimaji wa Songea, Bahatisha Ndulute yeye aliidakia Ushirika ya Moshi, Sahau Kambi, Yanga, Athumani Msumari yeye aliidakia Reli ya Morogoro.

Zamani nchi hii ilijaaliwa kuwa na makipa wengi mahiri na hata makocha wa timu ya taifa walikuwa wakikuna vichwa jinsi ya kuteua nani aitwe na nani aachwe.

Walikuwa makipa wenye uwezo mkubwa. Sasa kila ukiamka, Aishi Manula anabaki kuwa kipa namba moja na timu ya taifa. Ni kwa sababu hakuna aina ya makipa wale wa zamani ambao wengi wao viwango vyao vilikuwa bora kiasi cha kupishana kwenye kuchaguliwa kwenye kikosi cha Taifa Stars.

Lakini kwa kukukumbusha tu kuna baadhi ya makipa hapa pamoja na uzuri wao, hawakuwahi kuchaguliwa kwenye timu ya taifa. Si kwa sababu walikuwa hawafai, la hasha. Ni kwa sababu waliokuwapo kwenye kikosi hicho waliendelea kupambana kung'ang'ania namba.

Na hata walipoondoka, baadaye walirejea tena.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Ajenda ya siri-7

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

**Na Adam Fungamwangoo**
**(0716 350534)**

MWAHIJA alishusha pumzi na kumtazama mgeni wake. "Wewe ni mjomba wa yule binti?" "Ndiyo Mwahija."

"Basi tu nikwambie, yule binti alikuja kununua kweli hapa dawa hizo. Miezi sita iliyopita hapa hapa. Na si mara ya kwanza. Ni mteja wangu, huwa anakuja hapa kununua tu dawa za kawaida, malaria, UTI, za kutuliza maumivu, ninashangaa siku hiyo kaja kununua hizo dawa ambazo hajawahi kununua hata siku moja."

"Alinunua tu, au alikuja na cheti cha daktari?" Akahoji. "Alikuja akiwa na cheti cha hospitali kabisa, zilikuwa ni aina tatu za dawa, moja ni ya kutuliza maumivu."

"Ni cha hospitali gani?" "Hapana, muda umekuwa mrefu na tunahudumia watu wengi, siwezi kukumbuka, cha ajabu dawa hizo ndizo zimekwenda kumuua yule baba na yeye ndiye aliyezinunua, mimi nimekwenda kutoa ushahidi huo mahakamani kama nilivyoona kutoka alipokuja kununua na kuondoka, huko kwingine waliendelea wengine."

Moyoni Eddy alifarijika kupata ushirikiano kutoka kwa Mwahija. Uzoefu wake kwenye mambo ya kipelelezi ulimsaidia sana. Kumpoza msichana yule hadi kujibu maswali atakavyo kwa staili ya kucheza naye kwa maneno matamu kwanza. Kwa mwingine ingekuwa ni kazi ngumu kwa jinsi mwanzoni alivyompokea mgeni huyo kwa kumnyali.


"Ni muda gani ulijua kuwa yule binti amefanya tukio hilo baada ya kununua dawa hapa?"

"Kiukweli nilianza kuona kwenye gazeti la Nipashe ikiripoti kuhusu kifo cha yule mzee na ikasemekana kuwa binti yule ndiye amemuua kwa kumwekea sumu kwenye chakula ambazo ni mchanganyiko wa dawa. Mimi namfahamu yule msichana na hata yule baba namfahamu. Unajua nilishtuka sana niliposikia hivyo. Nililia sana na hata hapa kazini sikuja wiki nzima."

"Kwa nini?" "Kwanza woga mwenzangu. Yaani niliogopa na mimi nitakamatwa kwa sababu nilijua kabisa itafuatiliwa ili kujua zile dawa zilinunuliwa wapi na nani kamuuzia yule binti.

"Pili nilimwonea huruma binti kwa kitu ambacho atafanywa au kuhukumiwa, vile vile baba yule namfahamu na familia yake, mara kwa mara wanakuja hapa au wanapita."

"Nyumbani kwake unapafahamu?" "Ndiyo. Wala siyo mbali sana na hapa, unatoka hapa, kuna njia pale ile paleee, unakwenda nayo moja kwa moja, mbele kule kuna nyumba ina geti jeusi, upande wa kushoto ndiyo hiyo hiyo." Mwahija alikuwa akijibu maswali na Eddy ambaye kwa uzoefu wake, alijua kabisa yalikuwa ni majibu sahihi.




**"Kiukweli nilianza kuona kwenye gazeti la Nipashe ikiripoti kuhusu kifo cha yule mzee na ikasemekana kuwa binti yule ndiye amemuua kwa kumwekea sumu kwenye chakula ambazo ni mchanganyiko wa dawa. Mimi namfahamu yule msichana na hata yule baba namfahamu. Unajua nilishtuka sana niliposikia hivyo. Nililia sana na hata hapa kazini sikuja wiki nzima."**

"Kama ulijificha nyumbani, ilikuwaje tena ukachukuliwa kwenda kutoa ushahidi mahahamani?"

"Mmmh, wewe maswali yako, mbona kama polisi? Au polisi wewe unanificha?"

Eddy alitabasamu. Tabasamu ambalo nia yake ilikuwa ni kumtomfanya Mwahija aingiwe na hofu. Aone kama yupo na mwanaume kama mwanaume mwingine yeyote.

"Ningekuwa askari polisi nisingekuja hivi nilivyokuja. Pia nisingekubali jinsi ulivyokuwa unaniangalia na kunijibu mwanzo. Ningejitambulisha kuwa mimi ni askari ili unipe heshima yangu, lakini mimi sikulaumu kwa uliochokifanya. Siku zote nyuki huwa mkali kwenye mzinga wa asali yake."

"Una maana gani?" Akauliza Mwahija, huku akiwa anajua kabisa Eddy alikuwa na maana gani.

"Hebu tuendelee na hili kwanza, hayo tutazungumza baadaye mama."

"Uliniuliza swali gani vile?" "Ilikuwaje hadi ukachukuliwa kwenda kutoa ushahidi?"

"Walikuja askari polisi kazini na kunitaka nitoe maelezo jinsi walivyokuja pale kununua zile dawa, hadi akaondoka. Tena waliniuliza swali kama lako kama alikuja na cheti cha hospitali. Tukawaambia na ushahidi pale, wakasema mimi niliyemuuliza ninatakiwa niwe tayari siku ya kutoa ushahidi mahakamani kwa sababu nitahitajika.

"Ndiyo siku hiyo wakaja kuniletea barua ya wito wa kwenda mahakamani, nikatoa kama ilivyokuwa, na ikafanana na yule daktari alivyosema kuwa dawa iliyomuua marehemu ilikuwa ni aina ile aliyokuja kununua kwenye duka letu hili." Alimaliza jibu lake akitegemea swali lingine.

Eddy alimtazama Mwahija. Ni utazamaji ambao ulimshangaza kidogo Mwahija.

Alidhani kuwa baada ya kujibu vile, basi angeweza kukasirika kwa sababu ya kuonekana kuchangia kifungo cha mpwa wake, lakini sivyo. Ni utazamaji ambao kwa mwanamke yeyote anayetazamwa vile na mwaume anajua tu kuna namna.

"Ninashukuru sana Bi Mwahija kwa ushirikiano wako kwangu. Sasa nimepata uhakika na ushahidi mzuri kuwa mpwa wangu Tina amefanya tukio hilo. Sisi kama familia hatuna mtu wa kumlaumu, ila tu nachoshangaa ni kwa nini binti mdogo kama yule ameamua kufanya vile. Kwa nini? Na wamemfanya nini?"

"Yaani wewe unawaza kama mimi. Ndiyo amefanya, lakini ni nini walichomkosea? Kitu gani ambacho yule msichana amefanyiwa kikubwa hadi kufanya vile?"

"Basi yameisha Mwahija, chochote utakachofikiria utakuwa unaumiza kichwa chako bure, hebu na sisi sasa tuongee yetu." Eddy alianza uchokozi.

"Yepi tena?" "Umesahau mara hii? Si nilikwambia kuna jambo limenileta, lakini kuna lingine limetokea hapa hapa?"

"Nakumbuka, haya lipi lililotokea." "Ni hivi Mwahija, naomba tu unipeleke nikaone nyumba ya tajiri wa mpwa wangu Tina. Na siyo nataka kuiona tu, lakini nataka niongozane na mrembo kama wewe. Nitakuwa mwenye bahati kubwa."

Mwahija aliangua kicheko kikubwa. "Wewe mwanaume una mambo. Una maneno kama umechelewa kutembea vile."

"Uko sahihi. Mimi nilichelewa sana kutembea. Na sababu kubwa haikuwa na ulazima wa mimi kuwahi kutembea wakati mbebaji ambaye ni mama yangu mzazi yupo hai. Nilianza kutembea mwenyewe wakati nilipowasikia baba na mama wakitaka kunipeleka kwa mganga wa kienyeji eti nachelewa sana kutembea.

Nikaona hii sasa nitapelekwa kweli kwa mganga, ngoja tu kesho niwafurahishe nitembee." Wakati akiongea hiyo, Mwahija alikuwa amekauka kwa kicheko, kiasi kwamba hata rafiki yake aliyekuwa anahudumua wateja aliposikia kicheko hicho alishangaa.

Eddy alifurahi kwani tayari kazi yake ilikuwa imeanza vizuri. Siyo kwamba hakujua kama Mwahija alikwenda kutoa ushahidi mahakamani. Alichotaka ni kuwa na uhakika na ushahidi kuwa ni kweli Tina alikwenda kununua dawa ambazo zilimuua Chilambo.

Hii kwake ingeweza kumsaidia anapoelekea kwenye upelelezi wake. Anatakiwa awe na uhakika na kila kitu ili kupata vielelezo sahihi.

Na wakati huo alikuwa anarekodi kupitia kifaa chake cha kunasa sauti kama vinavyotumiwa na waandishi wa habari kuhoji watu. Lakini hili ni kifaa kidogo ambacho huwa hakionekani kirahisi. Kinakaa mfukoni tu. Mwahija yeye alikuwa alionekana kupata rafiki mcheshi. Mwenye maneno matamu ya kuvutia. Mtu ambaye hachoshi kumsikiliza. Pamoja na kwamba alikuja kuulizia habari za mpwa wake na kumpa ukweli, hakuonekana kusononeka, wala kumkasirikia. Ndiyo kwanza anamuomba ampeleke akaione nyumba ya marehemu Chilambo ambayo kwa sasa inaishi familia yake.

Mwanzoni alihofu kuwa inawezekana ni njama ya mtu yule ili alipize kisasi cha mpwa wake. Lakini moyo wake ulikataa. Ilitokea tu ghafla akaanza kumwamini mtu yule. Hakujua kwa nini.

"Da' Fatuma, natoka kidogo, nampeleka mgeni wangu hapo mbele, narudi sasa hivi." Ilikuwa ni sauti ya Mwahija akimuaga mwenzake aliyekuwa naye kwenye duka hilo.

INAENDELEA JUMAPILI



# NANDY AKEMEA KINACHOENDELEA TUZO AFRIMA

MWANAMUZIKI wa kike anayefanya vizuri katika Bongo Fleva,Nandy, amesema kinachoendelea katika tuzo za Afrima ni mambo ya kutisha nchini Nigeria.

Nandy amesema kabla ya tuzo hizo wasanii wa Kitanzania walipokelewa vibaya kiasi ambacho baadhi yao kama Zuchu alitakiwa kuondolewa katika jukwaa la mazoezi na yeye kukosa sehemu ya kulala.

"Unajua kilichoendelea kule Nigeria ni mambo ya hovyo, Watanzania sasa tunatakiwa kuwa wamoja katika kupigania jambo hilo, tumepokelewa vibaya sana na kila mtu alikosa raha na kujiona kama tumetengwa," amesema Nandy.

## Zlatan azidi kuweka rekodi

MWANAMUZIKI wa miondoko ya Zanku kutoka nchini Nigeria, Zlatan Ibile, ameendelea kushika nafasi za juu kwenye majukwaa mbalimbali ya kidigitali ya kuuza, kusikiliza na kupakua muziki duniani.

Albam yake ya Resen imekuwa ikinunuliwa kwa kasi katika majukwaa hayo ya muziki kama Apple Music, Spotify, YouTube Music, Deezer, Audiomack na Boomplay.

Zlatan amesema jina la albamu hiyo inatokana na neno la Kisweden lenye maana "Safari", imeonekana kupagawisha mashabiki wake na hata ziara yake nchini Uingereza, alifanikiwa kujaza uwanja wa O2 Academy.



## Nay wa Mitego unalalamika nini?

RAPA mwenye utata Nay wa Mitego, ameachia video ya wimbo wake mpya 'Acha Niongee' ambao unazidi kujadiliwa kila kona kutokana na ujumbe mzito uliokuwemo.

Video hiyo ambayo anaonekana Nay wa Mitego, yupo Gerezani umeanza kusambaa katika mitandao ya kijamii tangu wiki iliyopita na kuibua hisia tofauti kutoka kwa mashabiki wake.

Ndani ya wimbo huo, rapa huyo analalamika kuhusu maisha anayopitia kwa sasa na kwamba anajiona kutengwa na wasanii wenzake kutokana na misimamo yake.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### VLAHOVIC ATAKIWA MAN CITY

KLABU ya Manchester City inamfuatilia mshambuliaji wa Fiorentina, MSerbia Dusan Vlahovic, 21. ***(La Repubblica)***

### TORRES KUTUA MAN

MAAFISA wa Barcelona wamefanya mazungumzo na Manchester City kuhusu kumsajili mshambuliaji wa Hispania, Ferran Torres, 21, wakati wa dirisha dogo la Januari. Torres amefunga mabao tisa na kutoa asisti tatu katika mechi 28 za ligi ya primia kwa City. ***(ESPN)***

### BARCA KUTOSAJILI

RAIS wa Barcelona, Jqoan Laporta amesema hali ya kifedha ya klabu hiyo ina maana kuwa hawawezi kufanya usajili.***(Marca)***

### EVERTON KIMENUKA

MWENYEKITI wa Everton, Bill Kenwright ameitisha kikao cha dharura cha bodi, huku mustakabali wa kocha, Rafael Benitez ukitarajiwa kujadiliwa. ***(Mirror)***

### SANCHES ATAKIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Lille na Ureno, Renato Sanches, 24, ambaye thamani yake inakadiriwa kuwa pauni milioni 34.***(Fichajes)***

### DAVID AWANIWA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Lille na Canada, Jonathan David, 21, yuko kwenye rada za Arsenal.

### CALVERT-LEWIN AWINDWA

ARSENAL inahusishwa na mpango wa kutaka kumsajili, mshambuliaji wa Everton, Dominic Calvert-Lewin. ***(London Evening Standard)***

### AZMOUN ATAKIWA EVERTON

EVERTON inafikiria kumsajili mshambuliaji wa Zenit St Petersburg na Iran, Sardar Azmoun, 26, ambaye hapo awali alikuwa akihusishwa na West Ham, Tottenham na Arsenal. ***(90min)***

### ERIKSEN KUKATIZA MKATABA

KIUNGO wa Inter Milan na Denmark, Christian Eriksen, 29, anakaribia kukatiza mkataba wake. Eriksen hajacheza tangu alipopatwa na mshtuko wa moyo kwenye Euro 2020. ***(calciomercato.com)***

### MBAPPE ANUKIA REAL

REAL Madrid wana uhakika kuwa watamsajili mshambuliaji wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe, 22, ambaye mkataba wake utakamilika msimu ujao. ***(AS)***

### STRUBER KUMSAIDIA RANGNICK

KLABU ya Manchester United inaweza kumuomba kocha wa New York Red Bulls, Gerhard Struber kuwa msaidizi wa Ralf Rangnick. Wawili hao walifanya kazi pamoja katika klabu ya Red Bull Salzburg. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RANGNICK: NAWEZA KUBAKI MAN UNITED

**●●● Asema yupo tayari kuendelea kuwa kocha hapo Old Trafford ingawa...**

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa muda wa Manchester United, Ralf Rangnick hajaondoa uwezekano wa kubakia kama kocha baada ya kipindi chake cha miezi sita kumalizika.

**Rangnick amechukua mikoba ya Ole Gunnar Solskjaer hadi mwishoni mwa msimu huu kabla ya kuingia kwenye mkataba wa miaka miwili ya kazi ya ushauri wa klabu hiyo.**

"Kama kila kitu kitakwenda sawa na yakatokea mapendekezo kama niliyofanya pale RB Leipzig mara mbili - hilo linaweza kuwa jambo zuri na kuendelea kufanya kazi kwa mwaka mmoja - lakini hilo ni jambo la kufikirika," alisema kocha huyo mwenye umri wa miaka 63 raia wa Ujerumani akiwambia waandishi wa habari.

Rangnick alikuwa pale kwenye dimba la Old Trafford Alhamisi kushuhudia United wakiwachapa Arsenal 3-2 kwenye Ligi Kuu na mchezo wake wa kwanza kuwa kwenye benchi utakuwa wa leo Jumapili dhidi ya Crystal Palace.

"Kwa watu ambao nimezungumza nao wamekuwa wazi kabisa kwamba, tunazungumzia mkataba wa miezi sita kama kocha," alisema.

"Hatujazungumza kuhusu nini kitatokea baada ya kipindi cha majira ya joto.

"Kwa sasa, nina uhakika watakuwa wanaangalia namna ya kutafuta kocha mpya.

"Kama watazungumza na mimi kuhusu hilo, tutaona.

"Kwangu mimi, sasa akili yangu ni kuhusu kushinda mechi inayofuata na hilo ndilo jukumu langu kubwa."

MECHI KALI
HOME
AWAY
MANCHESTER UTD
1.62 | 3.96 | 5.28
CRYSTAL PALACE
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa
CHEZA USHINDE KASINO



# XAVI: DEMBELE NI BORA KULIKO MBAPPE

**BARCELONA,** Hispania

XAVI amedai Ousmane Dembele anaweza kuwa "mchezaji bora duniani katika nafasi yake" baada ya rais wa Barcelona, Joan Laporta kubainisha kwamba, fowadi huyo ni bora zaidi kuliko Kylian Mbappe.

Dembele, ambaye alisajiliwa kwa euro milioni 105 kutoka Borussia Dortmund mwaka 2017, mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu na amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka hapo Camp Nou, Januari.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa atakuwa huru kujadiliana na timu yoyote mwezi ujao kama hawatafikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya pale Barca.

Laporta alibainisha Alhamisi kwamba, mazungumzo yanakwenda taratibu tofauti na ilivyotarajiwa, lakini siku iliyofuata alisema kwamba, nyota huyo mwenye umri wa miaka 24 anataka kubakia hapo na ameambia TV3 ana amini fowadi huyo ni bora kuliko Mbappe.

"Tuna mahusiano mazuri na Dembele na anataka kubaki," alisema Laporta.

"Nina imani na Dembele. Yeye ni mchezaji bora kuliko Mbappe."



# Beki wa Arsenal amdunda mwizi wa gar

**LONDON,** England

NYOTA wa Klabu ya Arsenal, Gabriel alikabiliana na mwizi aliyebeba rungu la mchezo wa baseball ambaye alijaribu kuiba gari lake.

Beki huyo wa Arsenal alifuatwa nyuma hadi nyumbani kwake eneo la Barnet London na watu watatu Agosti 20 waliomtaka kuwapatia funguo za gari lake.

Kanda ya video ya tukio hilo inamuonesha Gabriel akijaribu kukabiliana na mtu aliyebeba rungu la mchezo wa baseball ambaye ba daye alijulikana kama Abdi Muse

Muse mwenye umri wa mial 26 alihukumiwa kifungo cha mial 5 jela kwa makosa ya wizi katil mahakama ya Harrow Crown N vemba 17.

Baada ya kuzidiwa nguvu mwi huyo alitoroka na funguo za gari Gabriel, lakini akaliacha gari hi nyuma katika gereji.

Baadaye jamaa huyo alikamatw na maafisa wa polisi na kushtakiw kwa wizi na kumiliki silaha hatar

HABARI MICHEZO

LIVE IN PLAY

# KOCHA MBEYA KWANZA AIPANIA COASTAL

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Mbeya Kwanza FC, Haruna Harerimana amesema ana imani na wachezaji wake na anaamini atapata pointi zote tatu kwenye mchezo dhidi ya Coastal Union.

Mbeya watakuwa wenyeji wa mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaopigwa leo katika uwanja wa Mkwakwani mjini Tanga.

Akizungumza na gazeti hili jana, Harerimana alisema hakuna mechi iliyokuwa rahisi iwe ugenini au nyumbani kikubwa kupata matokeo inategemea na maandalizi ya kikosi chake.

Alisema kutokana na ugumu wa ligi msimu huu kila mmoja anahitaji kushinda mechi zake, na yeye ana imani kubwa ya kupata matokeo chanya katika mchezo huo.

"Tunatambua ubora wa Coastal Union na tutaongeza umakini kuhakikisha tunatumia madhaifu yao kuweza kupata matokeo chanya," alisema Harerimana.

Alisema tayari amefanyia kazi mapungufu yao ikiwemo kupoteza dakika za mwazo huku na mabeki kuruhusu bao na kuwa na wakati mgumu kipindi cha pili kutafuta kusawazisha na kupata ushindi.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), Erick Hamis (kulia), akikabidhi kikombe cha ushindi kwa Bariki Marungu, katika hafla fupi ya kukabidhiwa vikombe vya ushindi wa michezo ya Shimmuta iliyofanyika Novemba mwaka huu mkoani Morogoro. **PICHA: BEATRICE SHAYO**



# Lwandamina kuamua hatima ya Dube

**Na Saada Akida**

HATIMA ya lini mshambuliaji wa Azam FC, Price Dube atarudi uwanjani ipo mikononi mwa Kocha Mkuu, George Lwandamina ambaye ndiye atakayeamua nyota huyo kuanza kucheza michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Azam, Vivier Bahati alisema Dube anaendelea vizuri na ameruhusiwa na daktari kufanya mazoezi ya uwanjani na wenzake.

Alisema kuhusu lini ataanza kucheza ni jukumu lao baada ya kuridhishwa na ufiti wa nyota huyo katika mazoezi na programu ya timu hiyo.

"Kucheza kwake kutategemea na ushauri wa daktari, maana tayari ameruhusiwa kufanya mazoezi ya uwanjani, benchi la ufundi sasa ndiyo lina maamuzi ya kumpangia mechi za kucheza na lini ataanza rasmi, baada ya kuwa fiti," alisema Vivier Bahati.

Alisema kikosi chao kinaendelea vizuri na maandalizi na wachezaji wote wako fiti isipokuwa, Iddy Nado ambaye aliumia kwenye mechi dhidi ya Mtibwa Sugar na yuko chini ya uangalizi wa madaktari.

"Hadi sasa ni Nado, anafanyiwa matibabu kilichokuwepo ni kumuombea arudi uwanjani mapema, wachezaji waliobakia wako fiti na wanaendelea na mazoezi kwa mechi ijayo dhidi ya Kagera Sugar," alisema Vivier.

SPORTPESA APP
BET LEO UWE MILIONEA



PAKUA SASA

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 05 - DESEMBA 2021


| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3799 | Manisa BBSK vs Kocaelispor | 1.82 | 3.42 | 3.86 |
| 13:30 | 4183 | Kayserispor vs Antalyaspor | 2.50 | 3.29 | 2.70 |
| 13:30 | 5119 | Umraniyespor vs Boluspor | 2.04 | 3.33 | 3.24 |
| 14:30 | 1082 | Bologna vs Fiorentina | 2.75 | 3.30 | 2.55 |
| 15:00 | 3871 | St Etienne vs Rennes | 3.98 | 3.73 | 1.83 |
| 15:00 | 4024 | Dundee Utd vs Celtic | 8.66 | 4.82 | 1.33 |
| 15:00 | 4324 | Zorya Lugansk vs FC Ingulets | 1.32 | 4.83 | 7.33 |
| 15:15 | 5218 | Rochdale vs Plymouth | 3.29 | 3.54 | 2.05 |
| 15:30 | 2259 | FK Napredak vs Red Star Belgrade | 19.32 | 6.76 | 1.11 |
| 15:30 | 5981 | Colchester vs Wigan | 3.74 | 3.55 | 1.90 |
| 16:00 | 3982 | Hatayspor vs Basaksehir | 2.43 | 3.40 | 2.71 |
| 16:00 | 5416 | Rayo Vallecano vs Espanyol | 2.15 | 3.19 | 3.54 |
| 16:15 | 1316 | FC Basel vs Lausanne-Sport | 1.45 | 4.72 | 5.70 |
| 16:30 | 1229 | GO Ahead Eagles vs Twente | 2.85 | 3.34 | 2.33 |
| 16:30 | 4033 | Dinamo Moscow vs Ufa | 1.54 | 4.04 | 5.51 |
| 17:00 | 1287 | Spezia vs Sassuolo | 3.20 | 3.70 | 2.09 |
| 17:00 | 2258 | Venezia vs Verona | 3.55 | 3.35 | 2.09 |
| 17:00 | 3296 | Lorient vs Nantes | 2.82 | 3.17 | 2.53 |
| 17:00 | 3436 | Montpellier vs Clermont Foot | 2.08 | 3.58 | 3.28 |
| 17:00 | 3840 | Monaco vs Metz | 1.37 | 4.88 | 7.57 |
| 17:00 | 3947 | Banik Ostrava vs Ceske Budejovice | 1.53 | 4.29 | 5.79 |
| 17:00 | 4062 | Reims vs Angers | 2.42 | 3.04 | 3.09 |
| 17:00 | 4392 | Leeds vs Brentford | 1.90 | 3.60 | 3.90 |
| 17:00 | 4552 | Manchester Utd vs Crystal Palace | 1.62 | 3.96 | 5.28 |
| 17:00 | 5408 | Tottenham vs Norwich City | 1.41 | 4.61 | 7.41 |
| 17:30 | 1933 | Stuttgart vs Hertha BSC | 2.21 | 3.29 | 3.24 |
| 17:30 | 2972 | QPR vs Stoke City | 2.35 | 3.23 | 2.89 |
| 18:00 | 1780 | Anderlecht vs Zulte Waregem | 1.23 | 6.12 | 9.87 |
| 18:00 | 2472 | Livingston vs Hearts | 3.65 | 3.21 | 2.04 |
| 18:00 | 3773 | Oleksandria vs FC Minaj | 1.60 | 4.04 | 4.42 |
| 18:15 | 4926 | Elche vs Cadiz CF | 2.03 | 3.09 | 4.09 |
| 18:15 | 5320 | Ionikos Nikea FC vs PAOK | 6.73 | 3.96 | 1.48 |
| 18:30 | 2925 | St. Gallen vs Grasshoppers | 2.33 | 3.51 | 2.77 |
| 18:45 | 2419 | Feyenoord vs Fortuna Sittard | 1.18 | 6.70 | 11.82 |
| 19:00 | 1231 | Stromsgodset vs Haugesund | 2.17 | 3.55 | 3.01 |
| 19:00 | 1477 | Molde vs Lillestrom | 1.36 | 5.13 | 6.90 |
| 19:00 | 2442 | Valerenga vs Mjondalen | 1.42 | 4.73 | 6.30 |
| 19:00 | 2931 | Sochi vs FC Krasnodar | 2.44 | 3.42 | 2.64 |
| 19:00 | 3990 | Fenerbahce vs Caykur Rizespor | 1.42 | 4.65 | 6.33 |
| 19:00 | 4257 | Nice vs Strasbourg | 1.84 | 3.63 | 4.07 |
| 19:00 | 5544 | Rapid Vienna vs Austria Vienna | 1.87 | 3.52 | 3.56 |
| 19:30 | 4044 | Aston Villa vs Leicester | 2.34 | 3.35 | 3.00 |
| 19:30 | 5142 | Monchengladbach vs SC Freiburg | 1.83 | 3.73 | 3.98 |
| 20:00 | 3073 | Randers vs Odense | 1.94 | 3.33 | 3.52 |
| 20:00 | 4106 | Sampdoria vs Lazio | 3.29 | 3.59 | 2.09 |
| 20:30 | 2301 | Levante vs Osasuna | 2.46 | 3.19 | 2.94 |
| 22:45 | 2134 | Bordeaux vs Lyon | 4.40 | 4.20 | 1.67 |
| 22:45 | 4135 | Juventus vs Genoa | 1.30 | 5.25 | 9.96 |
| 23:00 | 1762 | Celta Vigo vs Valencia | 2.10 | 3.35 | 3.50 |
| 23:30 | 2619 | Sporting Braga vs GD Estoril | 1.48 | 4.26 | 6.14 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


Michezo

Jumapili Desemba 5, 2021

Nipashe



Rangnick: Naweza kubaki Man United HABARI UK 21



Nyota wa Chelsea, Hakim Ziyech (kulia) akichuana na mchezaji wa West Ham kwenye mchezo wa Ligi Kuu England baina ya timu hizo jana. **PICHA: MTANDAO**

## Nabi akabidhi majina matatu Yanga

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi akiweka maandalizi sawa kuelekea pambano la watani wa jadi Simba, tayari uongozi wa timu hiyo umepokea majina ya nafasi tatu kwa ajili ya usajili wa dirisha dogo la usajili linalotarajiwa kufunguliwa Desemba 15, mwaka huu.

Taarifa zilizolifikia gazeti hili jana kutoka ndani ya klabu hiyo, zinasema Nabi anahitaji kupata matokeo chanya katika michezo iliyopo mbele yake ikiwemo dhidi ya Simba, lakini tayari hivi karibuni amekabidhi majina na nafasi za wachezaji ambao anataka kuwaongeza.

Mtoa habari huyo alisema nafasi anayohitaji kuongeza ni mshambuliaji wa kati na kiungo mchezeshaji na kupiga hesabu za kuongeza kipa mmoja mzawa huku kipa wa Mtibwa Sugar, Aboutwalib Mshery akitajwa.

"Tayari uongozi umeanza mchakato wa kufanyia kazi yale ambayo kocha Nabi anayahitaji katika usajili akichia jukumu hilo kwa viongozi, naye anafanya maandalizi ya kiufundi na mbinu kwa ajili ya pambano letu dhidi ya Simba," alisema Mtoa habari huyo.

Alisema msimu huu wamedhamiria na moja ya kikao cha kocha huyo na mdhamini wao kilisisitiza timu hiyo iwe inafanya vizuri na inatwaa ubingwa wa ligi kuu na kombe la FA.

Mtoa habari huyo alisema tayari suala la usajili linaanza kufanyiwa kazi kwa kuhakikisha wana imarisha kikosi chao kwa ajili ya kufikia malengo yao hayo.

Wakati viongozi wakiwa katika mchakato wa usajili, Nabi alisema anahitaji kufanya vizuri katika kila mechi ili kufikia malengo yao baada ya kupata alama nne katika michezo miwili, sasa wanapambana kupata ushindi katika mchezo dhidi ya Simba.

# Simba kumaliza kazi Zambia leo

**Na Adam Fungamwango**

## Kocha Franco amesema mechi itakuwa ngumu, lakini amejipanga kupambana kwani...

WAWAKILISHI pekee wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, Simba, leo watakuwa ugenini kwenye Uwanja wa Lusaka nchini Zambia, kucheza mechi ya marudiano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Red Arrows.

**Simba itaingia uwanjani ikiwa na mtaji wa mabao 3-0 ilioupata kwenye mechi ya mkondo wa kwanza iliyochezwa Jumapili iliyopita, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Kwenye mechi hiyo inayotarajiwa kuwa ngumu, Simba inatakiwa kushinda, kutoka sare yoyote ile, au kufungwa mabao yasiyosidi mawili ili kutinga hatua ya makundi.

Ni michuano ambayo Simba ilishawahi kufika fainali mwaka 1993, ilipofungwa na Stella Abdijan ya Ivory Coast kwenye Uwanja wa Uhuru (zamani Taifa) mabao 2-0, ambapo kabla Simba ilitoa suluhu ugenini kwenye mechi ya kwanza. Wakati huo ilikuwa inachezwa kwa mfumo wa mtoano mwanzo hadi mwisho.

Simba inacheza michuano ya Shirikisho barani Afrika, baada ya kung'olewa kwenye Ligi ya Mabingwa kwa mabao ya ugenini, ikishinda mabao 2-0 dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana, lakini ikakubali kipigo cha mabao 3-1 nyumbani, Uwanja wa Benjamin Mkapa, matokeo yakawa mabao 3-3, lakini wageni wakasonga mbele kwa kushinda mabao mengi ugenini.

Kocha Mkuu, Pablo Franco amesema mechi ya leo itakuwa ngumu, lakini amejipanga kupambana kwani wana wachezaji wazuri, lakini pia wakienda kucheza kwenye kiwanja kizuri pia.

"Najua mechi itakuwa ngumu na ninawaheshimu wapinzani wangu, ni timu nzuri na walionyesha hivyo kwenye mechi ya kwanza," alisema.

"Sasa watakuwa nyumbani, hawana cha kupoteza, watashambulia sana, inatakiwa tuwe makini," alisema kocha huyo raia wa Hispania.

Alisema kuwa kwenye mechi ya leo watacheza kwa kujaribu kuzuia mianya, lakini wakicheza mfumo wa kuubana uwanja kwa viungo wakabaji na mabeki kutawaachia wapinzani nafasi kubwa ya kumiliki mpira.

"Tunajua tukishinda tunakwenda kwenye hatua ya makundi. Tuna mtaji wa mabao 3-0, lakini hata tulivyocheza nyumbani hatukucheza kwenye kiwango chetu kutokana na hali ya hewa ya mvua," alisema.

Rally Bwalya, mchezaji raia wa Zambia ambako mechi inachezwa amesema wanaingia kwa kutowadharau wapinzani, lakini yeye amerejea hapo kuisaidia timu ya Simba na si vinginevyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042